SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

WIZARA YA MAJI, NISHATI NA MADINI

# HOTUBA YA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2025/2026

ILIYOWASILISHWA NA
MHE. SHAIB HASSAN KADUARA [MBM]
WAZIRI WA MAJI, NISHATI NA MADINI




JUNI, 2025

**SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR**

# HOTUBA YA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA MAJI, NISHATI NA MADINI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026


**MHE. SHAIB HASSAN KADUARA**

**WAZIRI WA MAJI, NISHATI NA MADINI**


**JUNI, 2025**

# YALIYOMO


YALIYOMO ........................................................................................... i

ORODHA YA VIAMBATISHO ........................................................................... ii

VIFUPISHO VYA MANENO ........................................................................... iii

1.0 UTANGULIZI ........................................................................................... 1

2.0 UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ZA WIZARA YA MAJI, NISHATI NA MADINI KWA KIPINDI CHA MIEZI TISA (JULAI – MACHI) KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 ........................................................... 3

3.0 MAFANIKIO YA UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ZA WIZARA KWA KIPINDI CHA JULAI – MACHI, 2024/2025 ......................................... 4

4.0 UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO .......................................... 31

5.0 MWELEKEO WA BAJETI YA WIZARA YA MAJI, NISHATI NA MADINI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 ........................................... 37

6.0 MAOMBI YA FEDHA KWA KAZI ZILIZOPANGWA KUTEKELEZWA KATIKA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 ..................................................... 42

7.0 HITIMISHO........................................................................................... 43

VIAMBATANISHO........................................................................................ 45

## ORODHA YA VIAMBATISHO

Kiambatisho Namba. 1: Mapitio ya Upatikanaji wa Fedha kwa Mwaka wa Fedha2024/2025 ........ 46
Kiambatisho Namba. 2:Vijiji vilivyopatiwa huduma ya umeme ........ 47
Kiambatisho Namba. 3: Maeneo yaliyokuwa na tatizo la umeme mdogo ambayo yameshapelekewa ya huduma za umeme ........ 48
Kiambatisho Namba. 4: Matokeo ya Residual Chlorine kwa skimu zilizokaguliwa ........ 49
Kiambatisho Namba. 5: Matokeo yaliyobainika katika ukaguzi wa vituo vikuu vya Umeme ........ 50
Kiambatisho Namba. 6: Hali ya uingizwaji na matumizi ya Mafuta (Lita) kwa Miezi Tisa (Julai - Machi) 2024/2025 ........ 52
Kiambatisho Namba. 7: Vituo vya mafuta kwa kipindi cha Julai - Machi, 2025 ........ 54
Kiambatisho Namba. 8: Mwenendo wa bei za Mafuta zilizotangazwa na Mamlaka kwa kipindi cha Julai - Machi, 2025 ........ 55
Kiambatisho Namba. 9: Gesi iliyoingizwa na kutumika kwa kipindi cha Julai - Machi, 2025 ........ 56
Kiambatisho Namba.10: Tani za Maliasili zilizochukuliwa kwa Kipindi cha Julai – Machi, 2025 Pemba ........ 57
Kiambatisho Namba. 11: Shughuli zilizotekelezwa kupitia Programu ya Uimarishaji wa Miundombinu ya Maji Zanzibar ........ 58
Kiambatisho Namba. 12: Shughuli zilizotekelezwa kupitia Mradi wa GiZ Julai-Machi, 2024/2025 ........ 60
Kiambatisho Namba. 13: Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 ........ 63

## VIFUPISHO VYA MANENO

| | |
|---|---|
| CCM | Chama cha Mapinduzi |
| CCTV | Closed Circuit Television |
| EPC+F | Engineering, Procurement, Construction + Finance |
| KV | Kilovoti |
| MW | Megawatt |
| NEC | National Energy Company |
| TV | Televisheni |
| TZS | Tanzania Shillings |
| USAID | United State Agency for International Development |
| VAT | Value Added Tax |

## 1.0 UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika,** naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu, kwa kutujaalia neema ya uhai, afya njema na uwezo wa kukutana hapa leo kwa lengo la kujadili Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Maji, Nishati na Madini kwa kipindi cha miezi tisa (Julai - Machi) 2024/2025 na Mwelekeo wa Makadirio ya Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 kwa dhamira ya kuendelea kuwatumikia wananchi wote wa Zanzibar.

2. **Mheshimiwa Spika,** napenda kumshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa ujasiri na uongozi wake imara katika kuleta maendeleo ya Taifa letu. Kupitia uongozi huo, ameonyesha umahiri katika kutupatia maelekezo ya kuhakikisha huduma za maji safi na nishati safi zinaendelea kuimarika.

3. **Mheshimiwa Spika,** aidha, namshukuru na kumpongeza Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa uongozi wake thabiti katika kukuza maendeleo ya nchi yetu, hususan katika sekta za Maji, Umeme, Afya, Elimu, Miundombinu na Uwekezaji. Kupitia uongozi wake tumeshuhudia miradi mingi ya kimkakati inayofanyika kwa kasi, ikiifanya Zanzibar kuwa mfano bora. Juhudi zake katika kuimarisha amani, ukusanyaji wa kodi na mahusiano ya kitaifa na kimataifa zimechangia ukuaji wa uchumi na huduma za kijamii na kuleta utulivu nchini.

4. **Mheshimiwa Spika,** kwa hakika Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa baraza la mapinduzi, amefanikiwa kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya Mwaka 2020-2025 kwa zaidi ya asilimia 100 na hatuna tunachomdai kwa awamu hii. Nawaomba Waheshimiwa Wawakilishi na wananchi wenzangu wote ifikapo Oktoba, 2025 twende kwa wingi kumchagua Rais wetu mpendwa Dkt. Hussen Ali Mwinyi na kukipa ushindi wa kishindo Chama cha Mapinduzi, ili kiendelee kuongoza Dola na kuwatumikia wananchi wa Zanzibar na kuwaletea maendeleo ya haraka zaidi.

5. **Mheshimiwa Spika,** vile vile, napenda kuchukua fursa hii kuwapongeza wasaidizi wake wakuu; Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Mheshimiwa Othman Masoud Othman na Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla, kwa namna wanavyoendelea na majukumu yao ya kumshauri vyema Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

6. **Mheshimiwa Spika,** nampongeza Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid Spika wa Baraza la Wawakilishi kwa uongozi wako bora, ambao umeleta ufanisi katika kutunga sheria na miswada ya kimaendeleo. Wizara yetu itaendelea kuthamini juhudi zako na tunakutakia kila la kheri katika majukumu yako. Kadhalika nampongeza dada yangu Mheshimiwa Mgeni Hassan Juma, Naibu Spika wa Baraza la Wawakilishi, mara nyingi amekua mweledi na mchapakazi katika kukusaidia shughuli mbali mbali za ndani ya Baraza.

7. **Mheshimiwa Spika,** nawashukuru na kuwapongeza Waheshimiwa Wenyeviti Baraza lako pamoja na Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Baraza hili. Pongezi za pekee kwa Mheshimiwa Yahya Rashid (Mamba), Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati na Mwakilishi wa Jimbo la Kwahani kwa busara na hekima zake katika uongozi wake.

8. **Mheshimiwa Spika,** nawapongeza Makamo Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Waheshimiwa Wajumbe wote kwa ushirikiano wao wa dhati na kazi nzuri. Mmenisaidia sana katika kufanikisha shughuli za wizara yetu na kuimarisha utoaji wa huduma bora kwa wananchi.

9. **Mheshimiwa Spika,** nampongeza dada yangu Mheshimiwa Zawadi Amour Nassor, Mwakilishi wa Jimbo la Konde na Naibu Waziri katika Wizara ya Maji, Nishati na Madini. Uchapakazi na ushupavu wako katika kupigania maendeleo ya wananchi ni wa kupongezwa. Nakuahidi kuendelea kushirikiana nawe katika kutatua changamoto zinazowakabili wananchi wetu.

10. **Mheshimiwa Spika,** naahidi mbele ya Baraza lako Tukufu kwamba nitaitumikia nafasi hii kwa uweledi na juhudi zangu zote. Nitajitahidi kuwatumikia wananchi na kuwaletea maendeleo hadi nihakikishe kwamba hakuna mwananchi anayeishi bila ya kupata huduma ya maji safi na salama, umeme pamoja na kuimarisha upataikanaji wa nishati ya mafuta na gesi salama hapa Zanzibar.

11. **Mheshimiwa Spika,** nawapongeza Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri kwa kuendelea kumsaidia Mheshimiwa Rais. Tunashuhudia maendeleo makubwa katika kila sekta, ikithibitisha usemi wa Rais wetu kwamba Yajayo ni Neema Tupu na Yajayo yenye neema yametimia. Nawatakia utekelezaji mzuri wa majukumu yenu, na Mungu awape afya njema na kila la kheri katika maisha yenu.

12. **Mheshimiwa Spika,** napenda kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Chake Chake kwa kuniunga mkono katika kipindi chote cha uwakilishi wangu. Ustahamilivu na uzalendo wao ni chachu ya kuimarika kwa huduma za jamii na uchumi katika jimbo letu. Niwaombe ndugu zangu tuendelee kushirikiana katika kulijenga Jimbo letu kupitia Chama Tawala CCM, ili maendeleo yazidi kuimarika.

13. **Mheshimiwa Spika,** nawapongeza wananchi kwa imani yao ya dhati katika kumuunga mkono Mheshimiwa Dkt. Hussen Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar. Wito wangu kwenu, wananchi wote kujitokeza kwa wingi Oktoba, 2025 kumuunga mkono Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussen Ali Mwinyi, ili kuwarejesha viongozi wetu na kuendelea kufaidi matunda ya maendeleo kama vile; Barabara, Skuli na Masoko ya kisasa katika kila kona ya nchi yetu.

14. **Mheshimiwa Spika,** baada ya utangulizi huo, naomba uniruhusu niwasilishe Taarifa ya Mapato, Matumizi, na Utekelezaji wa Wizara ya Maji, Nishati na Madini kwa kipindi cha Julai – Machi 2024/2025, pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

## 2.0 UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ZA WIZARA YA MAJI, NISHATI NA MADINI KWA KIPINDI CHA MIEZI TISA (JULAI – MACHI) KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

***Bajeti ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha, 2024/2025***

**Upatikanaji wa Fedha**

15. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Wizara ya Maji, Nishati na Madini (Fungu N03) iliidhinishiwa TZS 379.48 Bilioni, ambapo TZS 13.60 Bilioni ni kwa kazi za kawaida na TZS 365.88 Bilioni kwa Miradi ya Maendeleo. Hadi tarehe 31 Machi 2025, Fungu N03 liliingiziwa TZS 96.71 Bilioni, sawa na asilimia 25.0. Kati ya hizo, TZS 9.46 Bilioni (asilimia 69.5) zilitumika kwa matumizi ya kawaida, na TZS 87.25 Bilioni (asilimia 23.8) kwa miradi, kama inavyoonyeshwa katika ***Kiambatisho Namba 1.***

16. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2024/2025 Wizara kupitia Maliasili Zisizorejesheka, ilipangiwa kukusanya TZS. 15.622. Bilioni ambapo Unguja ilitarajiwa kukusanya **TZS 13.600 Bilioni** na Pemba **TZS 2.022 Bilioni**. Hadi tarehe 31 Machi 2025, Wizara imefanikiwa kukusanya **TZS 17.32 Bilioni,** sawa na asilimia **111** ya makadirio. Kati ya hizo, Unguja imekusanya **TZS 16.10 Bilioni** (asilimia 118), na Pemba **TZS 1.22 Bilioni** (asilimia 60). Mafanikio haya yanatokana na usimamizi na udhibiti mzuri wa rasilimali za mchanga, matumizi ya kielektroniki kutoa vibali, na adhabu kwa wanaokiuka utaratibu wa maliasili zisizorejesheka.

## 3.0 MAFANIKIO YA UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ZA WIZARA KWA KIPINDI CHA JULAI – MACHI, 2024/2025

17. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Wizara ilitekeleza bajeti yake kwa kuzingatia vipaumbele vifuatavyo: -

    i. Kuimarisha miundombinu ya usambazaji wa huduma ya umeme na maji;

    ii. Kudhibiti wizi wa umeme, miundombinu ya maji pamoja na uvamizi na uharibifu wa vyanzo vya maji;

    iii. Kuimarisha nyenzo za udhibiti wa huduma za maji na nishati;

    iv. Kufanya tafiti kwa lengo la kuimarisha huduma za sekta zinazosimamiwa na Wizara;

    v. Kuwatambua, kuwasajili na kuwafungia mita wateja wapya na wa zamani wanaopata huduma ya maji; na

    vi. Kuimarisha upatikanaji wa huduma ya Maji safi, Nishati na Madini kwa kutekeleza miradi mikubwa ya kimkakati.

***Sekta ya Maji (Hali ya Sekta ya Maji Nchini)***

18. **Mheshimiwa Spika,** Sekta ya maji ni miongoni mwa sekta muhimu kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii ndani ya nchi. Umuhimu na thamani ya maji huonekana kutokana na kukua kwa kasi ya mahitaji ya shughuli za maendeleo na kijamii zinazoibuka kila siku. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imefanya juhudi kubwa za kuhakikisha huduma hii inapatikana kwa ufanisi.

19. **Mheshimiwa Spika,** hadi Machi, 2025 uzalishaji wa maji safi na salama Unguja umefikia lita 154,808,220 (Mkoa wa Mjini Magharibi uzalishaji umefikia lita 107,024,400, Mkoa wa Kaskazini Unguja uzalishaji umefikia lita 20,361,600 na Mkoa wa Kusini Unguja uzalishaji umefikia lita 27,422,220) kwa siku. Mahitaji ya maji kwa Kisiwa cha Unguja ni lita 190,938,860 (Mkoa wa Mjini Magharibi mahitaji umefikia lita 125,043,660, Mkoa wa Kaskazini Unguja mahitaji umefikia lita 36,020,600 na Mkoa wa Kusini Unguja mahitaji umefikia lita 29,874,600) kwa siku. Hali hii inapelekea upungufu wa lita 36,130,640 kwa Unguja (Mkoa wa Mjini Magharibi mapungufu ya lita 18,019,260, Kaskazini Unguja mapungufu lita 15,659,000 na Mkoa wa Kusini Unguja mapungufu lita 2,452,380) kwa siku.

20. **Mheshimiwa Spika,** hali halisi ya uzalishaji wa maji safi na salama Pemba imefikia lita 56,298,547. (Mkoa wa Kaskazini lita 25,453,747 na Kusini lita 30,844,800) kwa siku. Mahitaji ya maji kwa Pemba ni lita 87,494,000 (Kaskazini Pemba lita 43,806,650 na Kusini Pemba lita 43,687,350) kwa siku. Hali hii inapelekea upungufu wa lita 31,195,453 kwa Pemba (Mkoa wa Kaskazini Pemba mapungufu ni lita 18,352,904 na Mkoa wa Kusini Pemba mapungufu lita 12,842,549) kwa siku.

21. **Mheshimiwa Spika,** kwa kushirikiana na Shirika la KfW, Wizara imepata msaada wa kuandaa Mpango Mkuu wa Maji Safi na Maji Taka pamoja na Mpango Mkuu wa Rasilimali Maji. Aidha, miongozo ya uendeshaji na usimamizi wa miundombinu ya maji katika sekta ya maji itaandaliwa. Mkataba wa kazi hii umesainiwa Disemba, 2024 na kazi inaendelea. Aidha, kupitia Shirika la Maendeleo GIZ, kutafanyika upembuzi yakinifu wa uvunaji wa maji ya mvua. Vile vile, Washirika wa Maendeleo SADC-GMI kwa kushirikiana na Global Water Partnership Tanzania wanafadhili kazi ya kufanya tathmini ya kiwango na ubora wa maji ya chini ya ardhi. Matokeo ya tathmini hii yatatuwezesha kupata mfumo wa ufuatiliaji na usimamizi wa rasilimali maji.

22. **Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha vyanzo vya maji vinadhibitiwa, Wizara imechukua hatua ya kuweka mabango 129 ya umiliki wa maeneo ya hifadhi ya vianzio vya maji katika maeneo yote ya Mradi wa Exim India. Aidha, Wizara imefanikiwa kujenga uzio katika visima viwili (2) vilivyopo Unguja Ukuu, ili kudhibiti uvamizi wa Hifadhi za vianzio vya maji unaosababishwa na shughuli za ujenzi wa makaazi. Zoezi hili litaendelea katika maeneo mengine ya vianzio vya maji Unguja na Pemba, kulingana na upatikanaji wa fedha.

23. **Mheshimiwa Spika,** Wizara, kupitia mradi wa Usimamizi wa Rasilimali Maji Ardhini unaofadhiliwa na Shirika la Maendeleo la Japan (JICA), itaanzisha mfumo wa ufuatiliaji wa rasilimali maji. Hii itajumuisha ununuzi na matumizi ya vifaa vya kisasa vya usimamizi wa vyanzo vya maji, kama vile *Telmetric probes* na *Multiparameter*, kwa ajili ya kuangalia ubora wa maji katika vyanzo vya Mkoa wa Mjini Magharibi ikiwa ni majaribio (Pilot).

24. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imeandaa programu ya kuondosha mabomba chakavu yenye urefu wa mita 645,372.32 katika Mkoa wa Mjini Magharibi na kuiwasilisha kwa kampuni ya Rand Water Zanzibar kwa ajili ya uhakiki, tathimini na utekelezaji. Sambamba na hilo, katika kuhakikisha wananchi wanapata maji safi na salama Wizara inaendelea na ununuzi wa mabomba kwa maeneo yaliyoathirika na ujenzi wa barabara. Aidha, Wizara tangu mwenzi Januari 2025 imeendelea kuwaunganishia maji wananchi katika maeneo yaliyopitiwa na mradi wa Exim India, ambapo hadi sasa jumla ya nyumba 7,845 mpya zimeunganishwa na huduma pamoja na kufungiwa mita. Kazi hii inaendelea katika maeneo mengine.

25. **Mheshimoiwa Spika,** Wizara inaendelea na juhudi za kuleta mageuzi makubwa katika sekta ya maji, na tayari tunaona matokeo yenye matumaini. Mageuzi haya yanafanywa kwa kushirikiana na kampuni ya Rand Water, ambayo inatekeleza kazi mbalimbali kuhakikisha huduma ya maji inakuwa endelevu. Tangu Rand Water kukabidhiwa rasmi mwishoni mwezi wa Februari 2025 hadi sasa, kampuni imefanikiwa kuziba mivujo 89 kati ya 145 Unguja na mivujo 106 kati ya 118 Pemba na kuokoa jumla ya lita 1,872m3 kwa siku.

26. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imefanikiwa kuratibu kikao cha pamoja na wataalamu kutoka Benki ya Dunia ili kujadili uboreshaji wa huduma katika sekta ya maji. Katika kikao hicho, Benki ya Dunia imekubali kutoa msaada wa kuandaa Andiko Yakinifu ya Usimamizi wa Maji Machafu Zanzibar ikiwa ni sehemu ya program ya ***Green Smart City Programme Tanzania,*** pamoja na kusaidia kuunda kamati maalumu ya uratibu wa washirika wa maendeleo katika sekta ya maji. Kwa kufanya hivyo, uwezo wa watendaji utaendelea kuimarika katika uratibu wa misaada ya kitaalamu na fedha kutoka kwa washirika wa maendeleo.

27. **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai – Machi, 2024/2025 Wizara imetekeleza Programu ya Usimamizi wa Huduma za Maji na kupata mafanikio yafuatayo: -

**Programu Kuu ya Usimamizi wa Huduma za Maji**

28. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii imetekelezwa na Idara ya Maendeleo ya Maji pamoja na Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) ambayo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 iliidhinishiwa kutumia jumla ya **TZS. 164,486,943,000** hadi Machi, 2025 programu ilitumia **TZS. 37,583,403,114** kwa ajili ya matumizi mengineyo, mishahara, ruzuku ya mishahara na kazi za miradi ya maendeleo.

***a) Idara ya Maendeleo ya Maji***

29. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imeandaa ramani ya miundombinu mikongwe ya mabomba katika Mkoa wa Mjini Magharibi kwa kipindi cha Julai-Machi, 2025. Ramani hii itasaidia kuweka kumbukumbu, kutatua changamoto za taarifa na takwimu za mtandao wa maji na kuepusha uharibifu wa miundombinu wakati wa ujenzi wa barabara na shughuli nyingine.

30. **Mheshimiwa Spika,** jumla ya mabomba yenye urefu wa mita 645,372.32 zimeibuliwa katika Mkoa wa Mjini Magharibi, ambapo awali zilikuwa hazijulikani. Kati ya hizo, mita 290,866.94 Wilaya ya Mjini, mita 248,020.85 Wilaya ya Magharibi "A" na mita 106,484.53 Wilaya ya Magharibi "B". Mabomba haya ni ya mtandao wa maji safi wenye kipenyo (diameter) cha sentimita 60.96 hadi 7.62.

31. **Mheshimiwa Spika,** aidha, kati ya mabomba hayo, yenye urefu wa mita 263,722.86 yanahitaji kufanyiwa ukarabati kutokana na uchakavu wa malighafi zilizotumika kufikia ukomo wa matumizi. Malighafi hizo ni polyethylene, polyvinyl chloride na mabomba ya saruji ya asbestose. Katika Wilaya ya Mjini, mabomba yenye urefu wa mita 121,621.01 yanahitaji ukarabati; Magharibi "A" mita 98,410.29, na Magharibi "B" mita 43,691.56 zinazohitaji ukarabati.

32. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imefanya tathmini ya upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama katika Mkoa wa Mjini Magharibi (shehia 121) na Kaskazini Unguja (shehia 75). Tathmini imeonyesha kuwa baadhi ya shehia hazijaunganishwa na mita za maji, hivyo wananchi wanapata huduma kupitia mfumo wa malipo ya "Flat Rate" au visima binafsi.

33. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imefanikiwa kusimamia Mradi wa Uimarishaji wa Miundombinu ya Maji katika Skimu ya Kengeja, ili kuhakikisha

upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama kwa wananchi wa Pemba. Hivi sasa, hatua inayoendelea ni ukarabati wa Tangi la Maji, kibanda cha pampu, na ulazaji wa mabomba. Kukamilika kwa mradi huu kutasaidia kuondoa changamoto za muda mrefu za upatikanaji wa maji katika Shehia ya Kengeja na Chonga.

34. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kwa kupitia Mamlaka ya Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) na kabla ya Rand water kukabidhiwa majukumu, imechukua hatua za kuunganisha huduma ya maji majumbani baada ya kukamilika kwa Mradi wa Exim-India. Hadi Disemba 2024, jumla ya nyumba 5,820 zimeunganishwa na huduma ya maji, ikiwemo Skimu ya Mkorogo (943), Maungani (1,458), Kidutani (750), Masingini (540) na Mfenesini (2,129). Lengo ni kuwapatia wananchi huduma ya maji safi na salama.

35. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imefanya majadiliano na mwekezaji wa mradi wa Kuimarisha huduma na miundombinu ya Maji Mkoa wa Kusini Unguja (*Rehabilitation and Upgrade of Water Infrastructure Project in Unguja South*), pamoja na kampuni ya Next Health Digital Solution BV (mshirika wa IT) na Dineshchandra R. Agrawal Infracon Private Limited (EPC Partner) kutoka Uholanzi na India. Mradi huu utaimarisha usambazaji wa maji safi na salama katika Skimu za Kizimkazi, Pagali, Jambiani na Bwejuu kwa mfumo wa uwekezaji binafsi wa (EPC+F). Aidha, Wizara imeandaa andiko la Programu Endelevu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji na Usafi wa Mazingira na kuwasilisha kwa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) kwa ufadhili.

### b) Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA)

36. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2024/2025 Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) ilipanga kukusanya **TZS. 10,870,491,200,** ambapo zinatokana na mauzo ya maji na Mapato menginenyo. Aidha, ZAWA ilipangiwa jumla ya **TZS. 9,134,300,000.00** kwa ajili ya ruzuku ya mshahara. Hadi kufikia machi, 2025 ZAWA ilikusanya jumla ya **TZS. 4,328,158,993.76** kutokana na mauzo ya maji na mapato mengineyo sawa na asilimia **39.82**. vile vile ZAWA ilipatiwa jumla ya **TZS. 6,475,377,977.57** sawa na asilimia **70.9** ya makadirio.

37. **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi hicho, Mamlaka imeendelea kutoa elimu kwa wananchi kupitia mikutano 38 ya uhamasisha ji (15 Unguja

na 23 Pemba) na kuandaa vipindi sita (6) vya habari kuhusu mafanikio ya Mheshimiwa Rais wa Zanzibar. jumla ya malalamiko 194 kuhusu maharibiko ya miundombinu ya maji yameripotiwa; kati yao, 26 ni kutoka mfumo wa Sema na Rais (SNR), ambapo 9 yamepatiwa ufumbuzi na malalamiko 168 yameripotiwa kwenye Afisi za Maji Unguja na Pemba ambapo malalamiko 153 yamepatiwa ufumbuzi.

38. **Mheshimiwa Spika,** ZAWA imeunganisha huduma ya maji safi kwa wateja wapya 15,889 (14,785 Unguja na 1,104 Pemba). Aidha, Utafiti wa uvutaji maji umefanyika kwa visima sita na matokeo yanaonyesha uzalishaji mzuri. Hatua inayofuata ni ujenzi wa vibanda na ulazaji wa bomba. Kadhalika, Mamlaka imesafisha visima 78 (21 Unguja na 57 Pemba) na kufunga pampu 46 (26 Unguja na 20 Pemba), isipokuwa Kisima cha Mchangani Mkiwa ambacho kitaanza kazi baada ya uunganishaji wa mtandao wa maji. Vile vile, Mamlaka imeziba mivujo 1,188 (508 Unguja na 680 Pemba) ili kuboresha upatikanaji wa maji safi na salama. Jumla ya mita 34,853.10 za mabomba zimewekwa (Unguja na Pemba).

39. **Mheshimiwa Spika,** jumla ya pampu 46 zimenunuliwa na kufungwa katika maeneo mbali mbali Unguja na Pemba, ambapo (10 Unguja katika kisima Jambiani Kijuuni, Mchangani Mkiwa, Mbweni Karume, Migombani Jeshini, Jendele Chwaka, Kaburi Kikombe, Mkorogo, Kianga kwa Mzee Juma, Muembe Mchomeke, Chumbuni na 20 Pemba (Jojo, Shangafu, Kiungoni Na. 1, Ng'ambwa (2), Sharifu Ali Na. 6, Matale, Mtuhaliwa, Manyaga, Bogoa, Wambaa skuli, Shidi, Mkanyageni, Uweleni darajani, Makangale no 1, Makangale Na. 2 covid 19, Wete- Taifu Na. 4, Matuleni Na. 1, Pagali Ikulu na Ng'ambwa Na. 2).

***Sekta ya Nishati (Hali ya Sekta ya Nishati Nchini)***

40. **Mheshimiwa Spika,** Zanzibar inapata huduma ya umeme kupitia waya za chini ya baharini kutoka Tanzania Bara. Unguja inatumia waya wa 45 MW ulowekwa mwaka 1980 na waya wa 100 MW ulowekwa mwaka 2013 kutoka Ras-Kiromoni hadi Ras-Fumba. Kwa upande wa Pemba, inatumia waya wa baharini wenye uwezo wa 20 MW kutoka Majani Mapana Tanga hadi Ras Mkumbuu, ambao unaendelea kutumika hadi sasa.

41. **Mheshimiwa Spika,** upatikanaji wa huduma ya umeme Zanzibar unaendelea kuimarika, ambapo hadi Machi 2025, jumla ya uniti 508,137,104.52 kWh

zimeuzwa kati ya 619,823,384.00 kWh zilizopangwa, sawa na asilimia 82 ya mauzo. Hii imepelekea mauzo ya jumla ya TZS 147,562,674,821.55, bila kujumuisha tozo ya VAT.

42. **Mheshimiwa Spika,** matumizi ya umeme yanaongezeka kutokana na kasi ya maendeleo nchini. Hadi tarehe 30 Machi 2025, mahitaji ya juu ya umeme Unguja yamefikia 136.4 MW (94.5 MW kwenye waya wa 100 MW na 41.9 MW kwenye waya wa 45 MW), sawa na asilimia 94 ya uwezo wa waya hizo. Kwa upande wa Pemba, mahitaji ya juu ni 16.70 MW, sawa na asilimia 84 ya uwezo wa waya wa 20 MW unaotumika.

43. **Mheshimiwa Spika,** katika kutoa huduma ya umeme kwa wananchi, sekta inakabiliwa na changamoto kadhaa, mojawapo ni upungufu wa kiwango cha voltage katika waya wa baharini unaoleta umeme kutoka TANESCO, unakabiliwa na mzigo mkubwa wakati wa matumizi ya juu ya umeme (peak demand), hali inayosababisha upungufu wa umeme, hasa kwa wateja walioko mwisho wa njia za usambazaji, kama vile Michamvi, Paje na Jambiani kwa Mkoa wa Kusini, pamoja na Nungwi, Matemwe na Kiwengwa kwa Mkoa wa Kaskazini. Umeme unaohitajika kutoka Tanzania Bara hadi Mtoni ni 132 kV, lakini kiwango kinachopokelewa Mtoni kwa muda mrefu kimekuwa kati ya 118 – 120 kV.

44. **Mheshimiwa Spika,** uwepo wa uchakavu wa miundombinu ni changamoto nyengine inayoikabili Shirika la Umeme Zanzibar. Aidha, nyaya mbili zinazopeleka umeme Kaskazini Unguja zimezidiwa na hivyo zinahitaji ukarabati na uwekezaji wa haraka. Hali hii inasababishwa na ongezeko la mahitaji ya umeme kutokana na kuunganisha wateja wapya wengi wa kawaida na wawekezaji huku miundombinu ikibaki kuwa ni ile ile.

45. **Mheshimiwa Spika,** licha ya changamoto hizo, tumeshuhudia kukatika kwa umeme mara kwa mara. Sababu za kukatika kwa umeme zimegawika katika makundi mawili: kukatika kwa umeme bila mpango (unplanned outage) na kukatika kwa umeme kwa mpango (planned outage). Hali hii inaathiri utekelezaji wa shughuli za kiuchumi na kijamii. Sababu nyengine zinazopelekea kukatika kwa umeme ni zifuatazo: -

i. **Kuzidiwa kwa mtandao wa kusambazia umeme:** Zanzibar inaendelea kushuhudia ukuaji wa kasi wa maendeleo unaotokana

na ujenzi wa miundombinu ya miradi ya kimkakati katika sekta mbalimbali ikiwemo; utalii, afya na elimu. Hata hivyo, ukuaji huo hauendi sambamba na maboresho ya miundombinu mipya ya umeme.

ii. **Athari za kimazingira:** laini nyingi za kusafirishia na kusambazia umeme zimezungukwa na mazingira hatarishi ikiwemo; kupitiwa na miti mikubwa, hali inayopelekea baadhi ya wakati kukosekana kwa huduma ya umeme kwa laini hizo kunatokana na kuangukiwa na miti hiyo.

iii. **Ujenzi wa Miundombinu ya Barabara:** Ujenzi wa barabara umekuwa ukiathiri miundombinu ya usambazaji wa umeme iliyopo juu na chini ya ardhi.

**Mikakati inayoendelea kutatua Changamoto za Sekta ya Nishati**

**46.** **Mheshimiwa Spika,** moja ya jitihada za kuboresha umeme Zanzibar ni mazungumzo na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kuhusu tatizo la umeme wa chini ya kiwango unaotoka Tanzania Bara kuja Unguja.

**47.** **Mheshimiwa Spika,** katika hatua nyengine, Wizara imeingia mkataba na Kampuni ya Novavis International ltd kuboresha mfumo wa umeme Zanzibar. Mradi huu upo katika hatua za mwisho na unajumuisha ufungaji wa Voltage Regulators, capacity bank na ufungaji wa kifaa cha STATCOM (*Static Synchronous Compensator)* katika eneo la Mtoni, ambacho kinatarajiwa kuanza majaribio hivi karibuni. Kukamilika kwa kazi hiyo, kutahakikisha voltage ya umeme kutoka Tanzania Bara inakuwa thabiti na ya kutosha.

**48.** **Mheshimiwa Spika,** Vile Vile, Wizara kupitia Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO) imeendelea kuboresha miundombinu ya kusambaza umeme kwa kuongeza njia mpya za usambazaji umeme kwa lengo la kupunguza mzigo kwenye laini zilizopo na kuongeza ufanisi wa usambazaji wa umeme. Njia hizo ni kama ifuatavyo: -

i. **Njia maalum ya kusambaza umeme kwa matumizi ya kituo cha Welezo,** ambayo inalenga kuhakikisha kituo hicho kinapata umeme wa uhakika wenye kutosheleza mahitaji.

ii. **Njia ya kusambaza umeme kutoka Chwaka hadi Charawe,** ambayo inalenga kupunguza mzigo kwenye laini ya Kusini, hivyo kuboresha upatikanaji wa umeme katika maeneo hayo.

iii. **Njia ya kusambaza umeme kutoka Fuoni hadi Kisakasaka** inalenga kusaidia kupunguza mzigo kwenye laini ya Fumba na hivyo kuongeza uthabiti wa mfumo wa umeme katika maeneo hayo.

iv. **Njia ya kusambaza umeme kutoka Mtoni hadi Mpendae,** kwa ajili ya kuongeza ufanisi wa usambazaji wa umeme katika eneo hilo.

**49. Mheshimiwa Spika,** kukamilika kwa njia hizi mpya za usambazaji kutasaidia kwa kiasi kikubwa kutatua changamoto ya kukatika kwa umeme mara kwa mara, na hivyo kuongeza ufanisi na uendelevu wa huduma kwa wananchi.

**50. Mheshimiwa Spika,** katika kukabiliana na changamoto ya ongezeko la mahitaji ya umeme, Wizara kupitia ZECO imeendelea kuimarisha Gridi ya Taifa kwa kupanua mtandao wa usambazaji umeme kwa kiwango cha 33KV na 11KV. Hadi Machi, 2025 jumla ya urefu wa mtandao wa kusafirisha umeme umefikia kilomita 3398.10 sawa na ongezeko la asilimia 106 ikilinganishwa na kilomita 1645 zilizofikiwa Machi, 2024. Aidha, Wizara imepanga Mkakati mahsusi wa kutatua changamoto za umeme mdogo katika visiwa vya Unguja na Pemba ambao unahusisha jitihada za muda mrefu, muda mfupi na muda wakati.

**51. Mheshimiwa Spika,** katika jitihada za muda mrefu, Wizara kupitia Mradi wa ZESTA inajenga laini ya Usafirishaji umeme wa 132 kV ambayo itasafirisha umeme katika maeneo ya Kaskazini na Kusini Unguja. Ujenzi huo unaenda sambamba na ujenzi wa Vituo vya kupoozea umeme katika eneo la Makunduchi, Mkoa wa Kusini na eneo la Matemwe, Mkoa wa Kaskazinii. Aidha, Mkandarasi wa ujenzi wa laini hizo na Vituo vya kupoozea umeme tayari yupo eneo la kazi (Site) na kazi inaendelea.

**52. Mheshimiwa Spika,** Wizara katika kuhakikisha Zanzibar ina vyanzo vyake vya ndani vya umeme inajenga kituo cha kuzalishia umeme wa Jua chenye uwezo wa 18 MW katika eneo la Makunduchi. Ujenzi huu unatekelezwa chini ya Mradi wa ZESTA kupitia fedha za mkopo wa Benki ya Dunia.

**53. Mheshimiwa Spika,** katika juhudi za kutambua na kutatua changamoto za ongezeko la mahitaji ya umeme Wizara imekamilisha kuandaa Mpango Mkuu wa mahitaji ya umeme wa mwaka 2025-2050 yaani ***"Zanzibar***

***Power Master Plan 2025-2050"***. Aidha, Wizara inashirikiana na Wizara ya Nishati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutekeleza mradi mpya wa kulaza way awa umeme Bahari chini ya ufadhili wa banki ya maendeleo ya Afrika (AfDB), na kwamba upembuzi yakinifu wa mradi wa kusafirisha umeme umekamilika, ukiwemo Megawati 200MW kwa mkondo wa volti 220kV kwa Unguja na Megawati 100MW kwa mkondo wa volti 132kV kwa Pemba. Mradi huu unafadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) na utatekelezwa kwa muda wa miaka mitano kuanzia 2024/2025 na sasa uko katika hatua za kutafuta mkandarasi. Mradi huu utahakikisha upatikanaji wa umeme wa uhakika kwa mahitaji ya sasa na ya baadaye.

54. **Mheshimiwa Spika,** Wizara katika Mkakati wake wa muda mfupi na kati wa kutatua changamoto za umeme Zanzibar, imechukua juhudi kadhaa. Miongoni mwa juhudi hizo ni kufanya mazungumzo na wawekezaji wa Nishati ya umeme, ambapo Wizara imewapatia muongozo wa hatua za kufuata, ili kufanikisha uwekezaji katika sekta hii muhimu. Kupitia mazungumzo hayo, Wizara imefanikiwa kuingia Mkataba wa Mauziano ya Umeme kupitia ZECO na Kampuni mbili ambazo ni: -

i. ***Kampuni ya Aseel,*** itakayozalisha umeme kwa kutumia Nishati ya nguvu za Upepo (*Wind Energy*) ya kiwango cha 200MW, ambapo kwa hatua ya awali itazalisha 100MW Unguja na 20MW Pemba Mkataba huu ulisainiwa tarehe 23 Januari, 2025.

ii. ***Kampuni ya NextGen,*** itakayozalisha umeme kwa kutumia Nishati ya nguvu za Jua (*Solar Energy*) ya kiwango cha 30MW pamoja na uhifadhi wa umeme huo (*Battery Storage*) ya kiwango cha 80MWh. Mkataba huu ulisainiwa tarehe 06 Febuari, 2025.

55. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kwa kushirikiana na ZECO imepanga kubadilisha waya wa zamani wa 45MW wa baharini na kuweka waya mpya wa 100MW ndani ya mwaka wa bajeti 2025/2026. Hii itasaidia kukidhi mahitaji yanayotarajiwa kuongezeka wakati utekelezaji wa mradi wa AfDB ukiendelea katika taratibu za utekelezaji wake.

56. **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai – Machi, 2024/2025 Programu Kuu ya Usimamizi wa Huduma ya Nishati na Madini ilitekelezwa na kupata mafanikio yafuatayo: -

**Programu Kuu ya Usimamizi wa Huduma ya Nishati na Madini**

**57. Mheshimiwa Spika,** Programu hii inatekelezwa kupitia Idara ya Nishati na Madini, Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA) pamoja na Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO) ambayo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 iliidhinishiwa kutumia jumla ya **TZS. 212,358,150,000** kwa ajili ya matumizi mengineyo, mishahara na kazi za maendeleo. Hadi Machi, 2024/2025 programu hii imetumia **TZS. 14,186,947,572** kwa ajili ya matumizi mengineyo, mishahara, miradi ya maendeleo na malipo ya "retention".

**a) Idara ya Nishati na Madini**

**58. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kutoa elimu kuhusu matumizi ya Nishati za Kisasa na Nishati Mbadala kupitia maonesho mbali mbali, ikiwemo Maonesho ya Kilimo ya Nanenane (1-14/08/2024, Wilaya ya Magharibi A), Tamasha la Kizimkazi (18-25/08/2024, Wilaya ya Kusini) na Maonesho ya Biashara ya kuadhimisha miaka 61 ya Mapinduzi ya Zanzibar (2-15/01/2025, Wilaya ya Magharibi B). Katika maonesho hayo, viongozi, wafanyakazi wa Taasisi, na wananchi mbali mbali walipata uelewa zaidi juu ya kazi na programu zinazotekelezwa na Wizara pamoja na matumizi sahihi ya nishati. Aidha, Wizara ilishiriki katika Kongamano la Wahandisi lililofanyika Dar es Salaam (02-07/09/2024) ambapo wahandisi walijifunza mwenendo na uvumbuzi mpya katika fani ya uhandisi, hasa matumizi ya akili bandia (AI).

**59. Mheshimiwa Spika,** Wizara ilishiriki Kongamano la Nishati Safi ya Kupikia ***"Energy Connect Conference & Exhibition"*** lililofanyika tarehe 16 hadi 18 Oktoba, 2024, Jijini Dar es Salaam. Kongamano hili lililenga kukuza uvumbuzi na ushirikiano katika upatikanaji wa nishati safi na endelevu. Ushiriki wa wataalamu wa Wizara ulitoa fursa ya kujifunza teknolojia za kisasa na kukutana na wawekezaji na mashirika ya kimataifa.

**60. Mheshimiwa Spika,** Wizara ilishiriki vikao vya majadiliano Disemba, 2024, kuhusu Mpango Mahsusi wa Nishati wa Taifa (*National Energy Compact*) Jijini Dar es Salaam. Aidha, Wizara ilishirikiana na Wizara ya Nishati SJMT katika maandalizi ya Mkutano wa Wakuu wa Nchi za Afrika kuhusu masuala ya Nishati, uliofanyika tarehe 28 Januari, 2025, ambapo Mpango huu ulisainiwa rasmi. Mpango huo unalenga kuwapatia umeme wananchi milioni 300 barani Afrika na Tanzania itanufaika kwa kuwapatia

umeme wananchi milioni 8. Mafanikio ya mkutano huu ni kielelezo kizuri cha ushirikiano ya Kisekta kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Zanzibar.

61. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imewapatia mafunzo wafanyakazi sita (6) kuhusu usimamizi wa gridi ya kisasa na mifumo ya umeme nchini India tarehe 15 hadi 28/08/2024, yaliyodhaminiwa na USAID na kuratibiwa na *Asia Foundation*. Mafunzo haya yameongeza ujuzi kwa wataalamu wetu katika usimamizi wa mifumo ya umeme, udhibiti wa huduma za nishati, na uunganishaji wa umeme wa jua katika gridi ya Taifa.

62. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kutoa mafunzo juu ya matumizi bora ya nishati, nishati mbadala ikiwemo nishati jadidifu na nishati safi ya kupikia kwa wanafunzi na walimu wa shule mbalimbali Unguja na Pemba, ambapo jumla ya skuli nane (8) zimepatiwa mafunzo hayo. Pia, Wizara ina mpango wa kuendeleza mafunzo haya kwa ngazi ya Masheha, Wilaya, Mikoa, na Taasisi za Serikali na Binafsi.

### b) Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO)

63. **Mheshimiwa Spika,** kwa kipindi cha Julai - Machi 2025, Shirika la Umeme limekusanya **TZS. 175.65 bilioni,** sawa na asilimia **103** ya makadirio ya **TZS. 170.10 bilioni.** Makusanyo haya yanatokana na mauzo ya umeme (TZS 136.90 bilioni), mapato mengineyo **TZS. 23.11 bilioni** na makusanyo ya madeni **TZS. 15.64 bilioni.** Mapato haya hayajajumuisha Kodi ya Ongezeko la Thamani wala kodi ya miundombinu.

64. **Mheshimiwa Spika,** Shirika la Umeme limepanga kufanya usambazaji wa huduma ya umeme katika vijiji 45, (27 Unguja na 18 Pemba). Hadi sasa, huduma ya umeme imepelekwa katika vijiji 31 (23 Unguja na 8 Pemba) kwa gharama ya **TZS 2.402 bilioni. Kiambatisho Namba. 2** kinaonesha vijiji hivyo.

65. **Mheshimiwa Spika,** Shirika la Umeme lilipanga kutumia **TZS. 178.27 bilioni** kwa uimarishaji na uendelezaji wa miundombinu ya umeme. Hadi sasa, Shirika limetumia **TZS 163.81 bilioni**, sawa na **asilimia 92**, kama ifuatavyo: -

i. Kubadilisha nguzo mbovu, 1393 (900 Unguja na 493 Pemba). Aidha, upatikanaji wa umeme wa kiwango kizuri umeimarishwa katika maeneo 39 (29 Unguja na 10 Pemba), sawa na asilimia 118 ya mpango wa kurekebisha umeme mdogo katika maeneo 33 (27 Unguja na 6 Pemba). Maelezo zaidi yanaonekana katika **Kiambatisho Namba 3.**

ii. Ukaguzi wa transfoma 747 (Unguja 495 na Pemba 252). Ukaguzi huo ni sawa na asilimia 46 ya transfoma 1635 (Unguja 1275 na Pemba 360) zilizopangwa kukaguliwa katika kipindi hicho. Kati ya transfoma 747 zilizokaguliwa, jumla ya transfoma 88 kwa Unguja na nne (4) kwa upande wa Pemba zilibainika kuwa na hitilafu na kufanyiwa masawazisho stahiki.

iii. Kuwaunganishia huduma ya umeme wateja wapya 25040 (21538 Unguja na 3,502 Pemba), ambapo ni sawa na asilimia 87 ya wateja 28800 (Unguja 23400 na Pemba 5400) waliopangwa kuunganishiwa umeme katika kipindi hicho.

## HALI YA MADENI YA WATEJA WA ZECO

**66. Mheshimiwa Spika,** Shirika la Umeme Zanzibar limekuwa likikabiliana na changamoto mbali mbali ikiwemo ya ukusanyaji wa madeni kutoka kwa wateja wake. Hali hiyo inatokana na utaratibu usioepukika wa matumizi ya umeme kabla ya malipo. Uwepo wa malimbikizo ya madeni kwa wateja wa Shirika la Umeme unatokana na baadhi ya wateja kushindwa kulipa ankara zao za matumizi ya umeme kwa ukamilifu na wakati. Hadi Machi 2025, Shirika linawadai wateja wake jumla ya **TZS. 73.7 Bilioni** ambapo mchanganuo wake unaonekana katika Jadweli lifuatalo.

***Jadweli linaonesha mchanganuo wa madeni ya umeme Unguja na Pemba hadi Machi 2025***

| Maelezo | Unguja | Pemba | Jumla |
|---|---|---|---|
| SMZ-ZAWA | 28,790,051,644.69 | 23,862,633,064.73 | 52,652,684,709.42 |
| SMZ NYENGINEZO + SMT | 11,504,222,482.06 | 1,602,868,278.34 | 13,107,090,760.40 |
| WATEJA BINAFSI | 7,873,378,197.86 | 106,748,045.63 | 7,980,126,243.49 |
| **JUMLA KUU** | **48,167,652,324.44** | **25,572,249,388.70** | **73,739,901,713.31** |

**67. Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Taasisi za Serikali (SMZ na SMT), Shirika limekuwa likifanya juhudi za kufanya vikao na Viongozi wa Taasisi hizo lakini bado baadhi ya Taasisi zimekua na muitiko mdogo wa kufanya malipo ipasavyo na kulikosesha Shirika mapato yake stahiki.

### c) Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA)

68. Mheshimiwa Spika, kwa kipindi cha Julai – Machi, 2024/2025, Mamlaka ilipanga kukusanya jumla ya **TZS. 19,876,439,625** hadi Machi, 2025 ilikusanya **TZS. 21,185,581,366.2** ambayo ni sawa na asilimia 107 ya makadirio kwa kipindi hicho. Aidha, Mamlaka ilipanga kutumia jumla ya **TZS. 21,185,581,366.2.** Matumizi halisi yalifikia jumla ya **TZS. 20,960,946,926.44** sawa na asilimia **98.9** ya makadirio kwa robo tatu. Kati ya fedha hizo, **TZS. 8,088,906,274.2** zilitumika kwa kazi za kawaida, **TZS. 312,040,652.24** kwa kazi za Mradi, **TZS. 5,000,000,000** zimeekezwa katika SUKUK ya Serikali na **TZS. 7,560,000,000** zilitumika katika mchango wa Mfuko Mkuu wa Serikali.

**69.** **Mheshimiwa Spika,** Mamlaka imeandaa nyenzo za udhibiti wa huduma za maji na nishati zikiwemo: Kanuni ya Utaratibu wa Ukusanyaji wa Ada na Tozo za Udhibiti (*Fees and levy Collection Regulations*) pamoja na Kanuni na Tafsiri ya Upakiaji na Ushushaji wa Mafuta (*Petroleum Off loarding and Back loarding Regulation*). Aidha, imefanya mapitio na kurekebisha Kanuni ya Wafanyakazi wa Mamlaka (*Staff Regulations)*. Imetayarisha Viashiria vya upimaji utendaji kazi vya Mtoa huduma wa Umeme (ZECO) baada ya kufanya mapitio ya bei za Umeme ya Zanzibar. Vile vile, imefanya mapitio ya nyenzo za ukaguzi wa miundombinu (Inspection Manual) na kufanya mapitio ya Kanuni ya Utatuzi wa Migogoro.

**70.** **Mheshimiwa Spika,** Mamlaka imeendelea na shughuli za ukaguzi wa ubora wa maji yanayosambazwa kwa watumiaji katika baadhi ya vyanzo na miundombinu ya maji kwa Wilaya za Unguja. Ukaguzi huo ulihusisha upimaji wa tabia za maji katika nyanja za *physiochemical parameters* ikijumuisha *Electrical Conductivity (EC)*, *Total Dissolved Solid (TDS), pH*, Temperature na *Residual chlorine.* Jadweli lifuatalo linahusika.

***Jadweli linaonesha Wilaya zilizofanyika ukaguzi***

| Eneo | Idadi ya Visima/Vituo vilivyokaguliwa ubora wa maji |
|---|---|
| Mkoa Kaskazini Unguja | 24 |
| Mkoa wa Mjini Magharibi | 24 |
| Mkoa wa Kusini Unguja | 7 |
| **Jumla** | **55** |

***Chanzo: ZURA, 2025***

71. **Mheshimiwa Spika,** matokeo ya ukaguzi huo, yameonesha kukidhi kwa viwango elekezi vilivyowekwa na Shirika la Afya Duniani (WHO) pamoja na Shirika la Viwango Zanzibar (ZBS) kwa vigezo (*water quality parameters*) vilivyopimwa na hivyo kukidhi viwango vya matumizi kwa binadamu.

72. **Mheshimiwa Spika,** kutokana na matokeo ya kaguzi zilizofanyika kuanzia robo ya kwanza, pili na tatu jadweli lifuatalo linaonesha mlinganisho wa kiwango cha chumvi kulingana na kota husika.

***Jadweli linaonesha mlinganisho wa kiwango cha chumvi (Electrical Conductivity, EC) kwa robo tatu (3) kwa Visima vyenye kiwango cha chumvi (EC) kinachozidi 1000 µS/cm***

| Chanzo cha Maji | Robo I | Robo II | Robo III |
|---|---|---|---|
| | EC (µS/cm) | EC (µS/cm) | EC (µS/cm) |
| Mtende | 1219 | 722 | 894 |
| Jambiani Kibigija | 1219 | 1084 | 1117 |
| Jambiani Mfumbwi | 1716 | 1725 | 1725 |
| Ukongoroni | 717 | 1240 | 1352 |
| Unguja Ukuu | 1058 | 982 | 1002 |
| Bwejuu | 1097 | 925 | 815 |
| Muyuni | 1160 | 1156 | 1153 |
| Matemwe mlilile | 2657 | 2813 | 2570 |
| Kisongoni | 1216 | 1210 | 1058 |
| **NB:** Kiwango kinachopendekezwa kwa matumizi ya binaadamu ni: - **EC < 2500 µS/cm (Viwango vya ZBS).** | | | |

***Chanzo: ZURA,2025***

**73. Mheshimiwa Spika,** ukaguzi umeendelea katika miundombinu ya maji katika Wilaya tano (5) zikijumuisha; Wilaya ya Kaskazini "A", Kaskazini "B", Kati, Kusini na Magharibi "A" ambapo vyanzo 101 vya uzalishaji maji vilikaguliwa. Aidha, kupitia ukaguzi wa marudio unaolenga kuangalia utatuzi na maboresho ya changamoto zilizobainika katika kaguzi za awali umeonesha 75% ya changamoto zilizobainika awali tayari zimerekebishwa.

**74. Mheshimiwa Spika,** ukaguzi wa kawaida katika Magharibi "A" – (Check Monitoring) umefanyika kwa kukaguwa vyanzo vya uzalishaji maji 29 pamoja na miundombinu yake. Matokeo ya ukaguzi huo yamebainisha kuwa visima tisa (9) havifanyi kazi kutokana na sababu za kuharibika kwa Pump na hitilafu za Control Pannel za kuwashia maji. Visima hivyo ni M/ Mchomeke, Kianga, N-4 na N-8 BHs, Selem I, Mfenesini BH, Mbweni Matrekta, Meli 4 Saccos, Dimani BH, Chunga – 026.

**75. Mheshimiwa Spika,** kadhalika, ukaguzi wa mitambo ya kutibia maji (*Water Treatment Plant*) na upimaji wa kiwango cha dawa ya kutibia maji ulifanyika katika skimu tano (5) za miradi ya maji ikijumuisha skimu za Dimani, Maungani, Mfenesini, Kidutani na Dole ambapo matokeo ya ukaguzi yamebainisha kuwa mitambo yote ya kutibia maji katika skimu zilizokaguliwa inafanyakazi kama ilivyokusudiwa na kiwango cha dawa kinaekwa kama viwango elekezi vinavoyelekeza. **Kiambatisho Namba. 4** kinafafanua.

**76. Mheshimiwa Spika,** Mamlaka imefanya ukaguzi wa miundombinu ya kusambazia umeme katika Mkoa wa Kusini Unguja (Wilaya ya Kusini na Wilaya ya Kati), Mjini na Mkoa wa Kaskazini Unguja kwa kuchagua maeneo tofauti ya njia za kusambazia umeme kwa lengo la kutambua hali halisi ya huduma inayotolewa kwa wananchi. Jumla ya vituo 112 vilikaguliwa katika mtandao wa Shirika la Umeme. Aidha, Mamlaka pia imefanya ukaguzi katika Vituo Vikuu vya kusambazia umeme na matokeo yake yanaonekana katika **Kiambatisho Namba. 5.**

**77. Mheshimiwa Spika,** vile vile, Mamlaka imefanya ukaguzi wa miundombinu ya Kituo cha Ras Kiromoni, kinachopokea njia mbili za kusafirishia umeme kutoka Kituo cha kupozea na kusafirisha Umeme cha Tegeta, laini hizo ni Zanzibar 1 (laini kongwe) pamoja na Zanzibar 2 (laini mpya) zenye msongo mkubwa wa 132kV, 45MW na 100MW kwa mfatano. Miundombimu ya kupokea umeme katika kituo hichi ni ya

kutumia *"overhead line"* na baadae laini hizo zilipitisha na kuunganishwa katika *"armed cable"* kwa lengo la kusafirishwa na kupita chini ya bahari hadi Ras Fumba (Zanzibar).

**78.** **Mheshimiwa Spika,** Mamlaka pia ilifanya ukaguzi katika Miradi mbali mbali ya Umeme wa Jua, ukiwemo mradi wa: -

***a. Hoteli ya Baraza Resort & Spa***

**79.** **Mheshimiwa Spika,** ukaguzi umefanyika katika eneo lililotekelezwa mradi wa uzalishaji umeme kwa kutumia nishati ya jua wenye uwezo wa kuzalisha 1MW lililopo Bwejuu. Ukaguzi umebaini kuwa, mradi huo unaendelea kuzalisha umeme katika hali ya kawaida na kupatiwa leseni mpya ya uzalishaji umeme.

***b. Matemwe Bungalows ZASWI (Z) Limited***

**80.** **Mheshimiwa Spika,** ukaguzi umefanyika katika eneo linalotarajiwa kuwekezwa mradi wa uzalishaji umeme kwa kutumia nishati ya jua baada ya kupokea maombi kutoka Kampuni ya MATEMWE BUNGALOWS ZASWI (Z) LIMITED, yenye lengo la kuzalisha 404kW. Ukaguzi umebaini eneo hilo linatosheleza kwa uwekezaji.

***c. Hoteli ya Mayai Ocean Resort***

**81.** **Mheshimiwa Spika,** ukaguzi umefanyika katika eneo lililowekezwa mradi wa uzalishaji umeme kwa kutumia nishati ya jua, ukaguzi ulifanyika na kuangalia miundombinu ya Umeme wa jua katika eneo la Bwejuu, ambapo wanatarajia kuzalisha wastani wa 29.2kW na kutumia katika hoteli yao ya *Mayai Ocean Resort.*

**82.** **Mheshimiwa Spika,** kupitia ukaguzi huo watendaji waliangalia miundombinu, ambapo paneli arobaini (40 PhotoVoltaic - PV) zimewekwa katika paa la jengo lao (Roof top) ambapo kila paneli moja ina wastani wa 730Wh. Vile vile, mradi huo unatumia Inverter tano zenye uwezo 11kW kwa kila moja sawa 55kW.

**83.** **Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ilikadiria kuingiza mafuta lita 195,000,000, ambapo kiwango halisi cha mafuta yaliyoingizwa nchini yalifikia lita 202,613,066, sawa na ongezeko la lita 7,613,066 ambapo sawa na asilimia 3.90 ya makadirio ya kipindi cha miezi Tisa. Kwa upande wa matumizi

jumla ya lita 193,776,526 yalitumika. Mchanganuo wa kila aina ya mafuta unaonekana katika **Kiambatisho Namba. 6.**

**84.** **Mheshimiwa Spika,** Mamlaka imeendelea kufanya ukaguzi wa Bohari saba (7), sita (6) kwa upande wa Unguja na moja (1) kwa Pemba pamoja na vituo vyote 117 vilikaguliwa. Kati ya vituo hiyo, 96 kwa Unguja na 21 kwa Pemba **Kiambatisho Namba.7** kinahusika.

**85.** **Mheshimiwa Spika,** Mamlaka kwa kushirikiana na Taasisi husika za Serikali imefanya ukaguzi wa maeneo ya ujenzi wa vituo vya mafuta, ambapo Jumla ya maeneo 9 yanayotarajiwa kujengwa vituo vya mafuta yalikaguliwa pamoja na Taasisi nyengine za Serikali. Kupitia ukaguzi huo, eneo moja tu la Mwera liliruhusiwa kukusanya nyaraka zinazohitajika ili kupatiwa kibali cha ujenzi. Maeneo yaliyokataliwa ni Muyuni mwabuani, Jambiani Kibigija, Barzenjy (Malindi, Ngalawa na Mangapwani), Mbuzini, Kizimkazi Dimbani na Michamvi.

**86.** **Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ilikagua bei za mafuta, ili kujiridhisha na bei halisi zilizotangazwa. Ukaguzi umeonyesha vituo vyote viliweka bei elekezi zilizotangazwa na Mamlaka **Kiambatisho Namba.8** kinafafanua.

**87.** **Mheshimiwa Spika,** kwa upande kusimamia uingizaji na matumizi ya Gesi ya Kupikia (LPG), kwa jumla kuna Kampuni nne (4) zinazoingiza na kuuza gesi kwa jumla katika visiwa vya Zanzibar, ambazo ni ORYX Gas Zanzibar Limited, Lake Gas LTD, Taifa Gas Zanzibar LTD na Al Nabahan Gas Supply (O-Gas). Aidha, kiwango cha Gesi kilichoingizwa nchini kwa kipindi cha Julai - Machi, 2025 ni kilogramu 8,594,238 na kiwango cha matumizi kimefikia kilogramu 9,260,910 **Kiambatisho Namba. 9 kinahusika.**

**88.** **Mheshimiwa Spika,** Mamlaka imeendelea kuratibu bei za gesi, bei hizo zinapangwa na kampuni zinazoingiza gesi kwa ujumla na kuridhiwa na Mamlaka. Bei hizo zinaonekana katika jadweli lifuatalo.

***Jadweli: Ujazo wa gesi na bei zake kwa kipindi cha Julai - Machi, 2025***

| UJAZO (KG) | BEI (TZS) (JULAI - MACHI) 2025 |
|---|---|
| 3 | 12,000 - 13,000 |
| 6 | 20,000 - 25,000 |
| 15 | 50,000 - 60,000 |
| 38 | 120,000 - 150,000 |

***Chanzo: ZURA, 2025***

**89.** **Mheshimiwa Spika,** Mamlaka imeendelea kutekeleza shughuli za uendeshaji, kuboresha uwezo wa Mamlaka pamoja na kuimarisha mazingira ya kazi na maslahi ya wafanyakazi kwa Kufanya matengenezo ya lifti, gari za ofisi pamoja na matengenezo madogo ya kisima cha Mamlaka Ziwani Polisi, Kufanya matengenezo makubwa ya Jengo la Mamlaka pamoja na upakaji wa rangi kwa jengo lote kwa nje. Vile vile, ilifanya tathmini ya zabuni nne (4) ambazo ni Zabuni ya Miundombinu ya Tehama, Vitendea kazi, Kutenganisha umeme na huduma za tiketi.

**90.** **Mheshimiwa Spika,** Mamlaka, imeendelea kutoa elimu kwa jamii kupitia vyombo vya habari na makongamano ya kijamii pamoja na kushughulikia malalamiko ya watumiaji wa huduma za Maji na Nishati. Ilifanya vikao na wadau wa maji kwa Unguja na Pemba na kuwasilisha Mfumo wa upimaji ufanisi (*Performance Benchmark*) pamoja na Viashiria vikuu (*Key Perfomrmance Indicators*) vya kupima huduma za maji. Imefanya vipindi vinne (4) vya redio kupitia ZBC Radio, Radio Jamii Kati, Mtegani na Tumbatu kuhusu mabadiliko ya bei za Umeme. Jumla ya Malalamiko 16 yamefanyiwa kazi na Mikutano tisa (9) kwa ajili ya kutatua Malalamiko kwa njia ya usuhulishi.

**91.** **Mheshimiwa Spika,** Mamlaka imeendelea kuwajibika katika shughuli za kijamii kwa kutoa misaada mbali mbali ikiwemo; Udhamini wa Tamasha la Vumba Festival 2024, Uchimbaji wa Kisima na Ujenzi wa Mnara pamoja na Ununuzi wa Mashine na Tanki la Maji kwa ajili ya wananchi wa Koani na Bwejuu Unguja, Ufadhili wa sherehe za Miaka 61 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar, Mradi wa hifadhi ya Maji na Mazingira, Msaada wa Vifaa vya Maji Jimbo la Chumbuni na Udhamini wa Uwasilishaji wa Ripoti ya utafiti wa Jiolojia na Madini. Aidha, imesaidia Uchimbaji wa Kisima kwa ajili ya wananchi wa Shungi Pemba.

92. **Mheshimiwa Spika,** Mamlaka kwa upande wa Pemba imekagua miundombinu ya maji katika Wilaya zote (Mkoani, Chake Chake, Wete na Micheweni). Aidha, jumla ya visima 114 vilikaguliwa ambapo katika Wilaya ya Mkoani, visima 41 katika Wilaya Chake Chake, visima 28 katika Wilaya ya Wete 31 na visima 14 vya wilaya ya Micheweni. Vile vile, kupitia eneo la Ukaguzi wa Ubora wa huduma ya maji jumla ya visima 46, vimekaguliwa. Kati ya hivyo visima 30 vipo Mkoa Kusini na visima 16 vipo Mkoa wa Kaskazini. Ukaguzi umebaini kuwa wastani wa taarifa zilizopatikana zimeonesha kuwa maji yanayosambazwa kwa wananchi yamekidhi vigezo na viwango "standards" vilivyowekwa na Taasisi ya Viwango Zanzibar (ZBS) na Taasisi ya Viwango Tanzania (TBS) hivyo kuyafanya maji hayo kufaa kwa matumizi ya binaadamu.

93. **Mheshimiwa Spika,** Mamlaka imekagua miundombinu ya umeme ikiwemo; Kituo cha kuzalishia umeme unaotokana na jua kilichopo Kokota, eneo la uwekezaji umeme wa jua liliopo Micheweni, baadhi ya transfoma na vituo vya kusafirishia umeme. Vile vile, imefanya ukaguzi katika Kituo cha Majani mapana kinachopokea umeme wa mkondo wa 132 kV kutoka Pangani na Hale na kinatumika kwa ajili ya kusambaza umeme katika maeneo tofauti ikiwemo Pemba kwa mkondo wa 33 kV.

94. **Mheshimiwa Spika,** Mamlaka pia imefanya ukaguzi katika kituo cha kuzalishia umeme unaotokana na nishati ya jua katika kisiwa cha Kokota kwa lengo la kubaini ufanisi katika kituo hicho. Matokeo ya ukaguzi yanaonesha kuwa, kituo cha Kokota kinaendelea kutoa huduma ya umeme kwa wananchi wa kisiwa hicho kikamilifu bila ya kuwepo kwa changamoto ya kukatika kwa umeme.

95. **Mheshimiwa Spika,** ukaguzi pia umefanyika katika kituo cha kuzalishia umeme unaotokana na nishati ya jua katika kisiwa cha Njao kwa lengo la kubaini mafanikio na mapungufu katika utoaji wa huduma kwa wananchi. Matokeo ya Ukaguzi umebaini kuwa, kituo hicho kinatoa huduma ya umeme kikamilifu bila ya kuwepo kwa changamoto ya kukatika. Eneo jengine la uwekezaji Micheweni lilikaguliwa, ambapo kuna muwekezaji wa umeme unaotokana na nishati ya jua amekaguliwa na kubaini majengo manne yamejengwa na kufikia hatua ya kuezekwa. Aidha, Mamlaka imefuatilia taarifa za umeme mdogo katika visima tisa (9) vya Maji vilivyopo Wilaya ya Chake - Chake. Ukaguzi ulifanyika wakati wa mchana

na usiku, ili kubaini kiwango cha umeme kinachoingia katika mitambo ya Maji kinatosha kuendesha mitambo hiyo.

96. **Mheshimiwa Spika,** Mamlaka imeendelea kutoa elimu kwa wadau kwa lengo la kuongeza uelewa juu ya masuala ya udhibiti wa maji na nishati. Mamlaka imefanya kikao na wadau wa maji kutoka Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) na kutoka Wizara ya Maji Nishati na Madini. Kikao hicho kilizungumzia Muongozo wa ufatiliaji na upimaji wa ubora wa maji, viashiria vya utendaji kazi (KPIs) na matokeo ya ukaguzi uliofanyika katika robo ya tatu ya Mwaka wa Fedha 2024/2025. Pia wadau walifahamishwa mafanikio na mapungufu yaliyobainika katika kaguzi zinazofanywa na ZURA. Changamoto zilizobainika waweze kuzifanyia kazi kwa lengo la kutoa huduma bora ya maji kwa wananchi.

97. **Mheshimiwa Spika,** aidha, ilitoa mafunzo kwa wauzaji wadogo 55 wa gesi ya kupikia (LPG) kisiwani Pemba juu ya muongozo wa maduka madogo ya gesi (LPG). Vile vile, imefanya kikao na wadau wa umeme wa kisiwani Pemba, Kikao kilipata fursa ya kuwasilisha matokeo ya ukaguzi wa miundombinu ya umeme uliyofanyika katika robo ya pili ya mwaka wa fedha, 2024/2025. Mafunzo kwa Masheha 129 kwa Wilaya zote za Pemba ambapo; Chake Chake (32), Mkoani (36), Wete (36) na Micheweni (25) pamoja na waandishi wa habari 12 wa vyombo vya umma na binafsi juu ya mabadiliko ya bei mpya za Umeme sambamba na majukumu ya ZURA.

**Sekta ya Madini**

98. **Mheshimiwa Spika,** hadi Machi, 2025 jumla ya maombi 764 ya leseni za kusafirisha Maliasili Zisizorejesheka yamepokelewa na kufanyiwa kazi pamoja na kupima gari kwa kutumia mizani wenye kuhamishika. Umuhimu wa kupima gari hizo unasaidia Serikali kujua kiwango halisi cha Maliasili Zisizoresheka kilichotumika nchini, kufuatilia ukusanyaji wa mapato yanayotokana na Maliasili hizo pamoja na kulinda miundombinu yetu ya barabara.

99. **Mheshimiwa Spika,** Wizara inaendelea kufanya doria katika maeneo mbali mbali ya Zanzibar pamoja na kufanya maboresho ya kikosi cha doria mara kwa mara, ili kuongeza ufanisi wa kazi. Lengo la doria hizo ni kudhibiti uchimbaji holela wa Maliasili Zisizorejesheka katika maeneo yote ya Zanzibar pamoja na kuzuia upotevu wa mapato. Hata hivyo,

jukumu la ulinzi wa Maliasili hizo ni mtambuka kuanzia kwa wananchi, Uongozi wa Shehia, Wilaya na Mkoa pamoja na Taasisi mbali mbali za Serikali ikiwemo Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira Zanzibar.

100. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kwa kushirikiana na Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania (GST) imefanikiwa kufanya utafiti wa miamba na kuandaa ripoti ya jiolojia ya Zanzibar iliyoambatana na ramani ya kijiolojia ambayo imezinduliwa rasmi na Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi tarehe 12 Septemba, 2024. Uzinduzi wa ripoti hiyo umefungua sura mpya ya uwekezaji katika sekta ya madini Zanzibar na kuelekea kuwa ni chanzo cha mapato katikakukuza Uchumi wa Zanzibar.

101. **Mheshimiwa Spika,** Wizara inaendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu sekta ya madini kwa kutumia njia mbali mbali ikiwemo; kuaanda vikao vya wadau ambapo Wizara ilifanikiwa kuwaongezea uelewa juu ya uratibu wa uchimbaji na usafirishaji wa Maliasili Zisizorejesheka Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya, Makatibu Tawala na Wakurugenzi wa Manispaa na Halmashauri Zanzibar. Kwa awamu ya pili Wizara ilifanikiwa kutoa elimu kwa Masheha wa Wilaya ya Kati kwa Unguja na Wilaya ya Micheweni na Mkoani kwa Pemba.

102. **Mheshimiwa Spika,** hata hivyo, Wizara imeendelea kutoa elimu kuhusu sekta ya madini kupitia maonesho ya kilimo ya nanenane yaliyofanyika tarehe 1 hadi 14/08/2024, Wilaya ya Magharibi A na Tamasha la Kizimkazi lililofanyika tarehe 18 hadi 25/08/2024, Wilaya ya Kusini, Unguja pamoja na Maonyesho ya Kuadhimisha miaka 61 ya Mapinduzi yaliofanyika Nyamanzi, Wilaya ya Magharibi B, Unguja ambapo Viongozi, Wafanyakazi wa Taasisi na wananchi walipata fursa ya kuongeza uelewa juu ya kazi na programu za Wizara pamoja na kujifunza masuala mbali mbali yanayohusu sekta ya madini.

103. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imenunua vifaa vya utafiti na ukaguzi wa Madini ambavyo vitasaidia katika tafiti mbali mbali za madini pamoja na ukaguzi ikiwemo Bandarini na Uwanja wa Ndege na kufanikiwa kuwapatia mafunzo mafupi ya matumizi ya vifaa hivyo watendaji wa Wizara. Vifaa ambavyo vilitolewa na Maafisa kutoka Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania (GST).

**Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Mipango ya WMNM**

104. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii inatekelezwa chini ya Idara ya Uendeshaji na Utumishi, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti pamoja na Afisi Kuu - Pemba. Kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, programu hii iliidhinishwa kutumia **TZS. 2,742,985,000** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na mishahara. Hadi Machi 2025, imetuma **TZS. 1,794,721,616** kwa matumizi mengineyo na mishahara.

**a) Idara ya Uendeshaji na Utumishi**

105. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ina jukumu la kuratibu na kusimamia Sheria, Kanuni na miongozo ya kiutumishi pamoja na kuhakikisha wafanyakazi wanapatiwa stahiki zao. Katika kulitekeleza hilo, Wizara imeendelea na hatua za kuimarisha mazingira ya kazi na wafanyakazi pamoja kuwapatia wafanyakazi stahiki zao kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Miongozo iliyowekwa. Miongoni mwa stahiki hizo ni mishahara, malipo ya kujikimu na malazi, mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi, likizo na kusimamia shughuli zote za Uendeshaji wa Ofisi.

106. **Mheshimiwa Spika**, aidha, Wizara imeratibu vikao mbali mbali ikiwemo vikao viwili (2) Kamati ya Uongozi, Vikao vitatu (3) Kamati Tendaji, Vikao viwili (2) Kamati ya Ukaguzi wa Hesabu za Ndani, Vikao 13 Bodi ya Zabuni pamoja na Kikao kimoja (1) cha wafanyakazi. Sambamba na hilo, Wizara imefanikiwa kuratibu na kusimamia mafunzo ya watumishi, jumla ya Watumishi 19 wamelipiwa ada ya mafunzo ya muda mfupi na wafanyakazi 12 wamepatiwa mafunzo ya muda mrefu. Vile vile, wafanyakazi mbali mbali wamepatiwa mafunzo ya uwelewa juu Rushwa na Uhujumu Uchumi, Mafunzo ya Sheria ya Utumishi wa Umma pamoja na Kanuni zake. Hii imepelekea kuongeza ufanisi kwa wafanyakazi katika kutekelezaji mjukumu yao.

**b) Idara ya Mipango, Sera na Utafiti**

107. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imekamilisha Sera ya Maji na Usafi wa Mazingira ya Mwaka 2025, iliyozinduliwa na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Hussein Ali Mwinyi, tarehe 22 Machi, 2025. Sera hii inaendelea kuleta mageuzi katika Sekta ya maji kwa kuimarisha upatikanaji wa huduma za maji safi na kudhibiti maji machafu. Aidha, Wizara imekamilisha mapitio ya Sera ya Nishati ya Mwaka 2009

na kuandaa Sera mpya ya Nishati ya Mwaka 2025. Sera hii ya Nishati tayari imeshakamilika na hatua inayofuata ni kuzinduliwa tuu rasmi kwa sera. Aidha, Wizara inaendelea kukamilisha uandaaji wa sera ya madini, ili kupata miongozo ya sera imara katika usimamizi na udhibiti wa sekta hii.

108. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imeandaa Mpango wa Kudhibiti Vihatarishi utakaosaidia kukabiliana na athari mbali mbali katika utekelezaji wa majukumu ya kisekta. Rasimu ya awali ya Mpango imetayarishwa na kuanza kutumika katika Mwaka wa Fedha 2025/2026.

109. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kwa kushirikiana na watendaji wa Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali inaendelea kukusanya takwimu, na kuzitengenezea utaratibu wa kuzichapisha na kuandaa kitabu cha takwimu zinazozalishwa na Wizara zikiwemo takwimu za maji, nishati na madini. Matarajio ya Wizara ni kutoa kitabu cha takwimu mwishoni mwa kila mwaka wa fedha husika. Aidha, kwa sasa Wizara ipo katika hatua za mwishoni za kukamilisha kitabu hicho.

110. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kwa kushirikiana na Taasisi ya Mashirikiano ya Maji Duniani kanda ya Tanzania (GWP-TZ) kupitia ufadhili wa Taasisi ya Usimamizi wa Maji ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC-GMI), imefanya utafiti wa kutathmini hali ya maji ardhini kwa upande wa Unguja na Pemba. Aidha, zoezi la awali la ukusanyaji wa taarifa (data) za utafiti huo limekamilika, hatua inayoendelea ni uchambuzi wa taarifa na kuandika ripoti ya utafiti huo. Aidha, kazi nyengine inayoendelea ni kuanzishwa kwa kanzidata itakayosaidia upatikanaji na uhifadhi wa taarifa sahihi kwa wakati zitakazosaidia katika kupanga, kusimamia, kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa majukumu ya Wizara katika utoaji wa huduma za maji, nishati na madini kwa wananchi.

111. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kwa kushirikiana na Taasisi ya Mashirikiano ya Maji Duniani kanda ya Tanzania (GWP-TZ) kupitia ufadhili wa Taasisi ya Uongozi, (Uongozi Institute), imefanya utafiti wa uvunaji wa maji ya mvua Zanzibar, ambapo ripoti ya awali imewasilishwa kwa wadau kwa majadiliano zaidi, na kujiridhisha na kukamilika mwisho wa mwaka huu wa fedha (2024/2025). Kukamilika kwa utafiti huo, kutaongeza uelewa na matumizi sahihi ya maji ya mvua kama ni rasilimali inayohitaji kuvunwa kwa manufaa ya kijamii na kiuchumi.

### c) Afisi Kuu - PEMBA

112. **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai-Machi, 2025, Afisi Kuu Pemba imeandaa na kuratibu vikao tisa (9) vya Wafanyakazi vyenye mnasaba wa kusikiliza changamoto zao na masuala ya usimamizi wa Rasilimali zisizorejesheka. Vile vile, imewapatia mafunzo ya muda mrefu wafanyakazi watatu (3), pamoja na kuwajengea uwezo wafanyakazi (18) kwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi ya Serikali mtandao (e-office).

113. **Mheshimiwa Spika,** aidha, Afisi Kuu imewapatia mafunzo ya doria wafanyakazi nane (8) pamoja na kuwapatia mafunzo elekezi (Induction course) wafanyakazi 18 kutoka Divisheni na vitengo tofauti. Sambamba na hilo, Afisi Kuu imeendelea kuimarisha mazingira ya kazi kwa Wafanyakazi kwa kusimamia Sheria na Kanuni za Utumishi wa Umma kwa kusimamia maslahi na kuwapatia Wafanyakazi stahiki zao, ikiwemo mishahara, muda wa ziada, likizo kwa wafanyakazi 16 na Kufanya tathmini ya utendaji kazi kwa wafanyakazi 20 kwa lengo la kuwapatia nyongeza zao.

114. **Mheshimiwa Spika,** vile vile, Afisi Kuu imekarabati barabara za kware ya Saninga na Kiungoni kwa kuweka fusi, ili kuwarahisisishia wachukuaji wa maliasili zisizorejesheka. Aidha, imerejesha maeneo yaliyochimbwa pamoja na kulipia fidia kwa wananchi walioathirika na shughuli hizo, imeboresha barabara ya Kiungoni na inatarajia kukamilisha barabara za kware mbili zilizobaki ambazo ni Saninga na Uwandani. Kadhalika, barabara ya kiungoni yenye urefu wa takriban kilomita 1.8 iliboreshwa kwa kujaliziwa fusi la tani 100 katika baadhi ya maeneo yaliyoonekana kuathirika zaidi na uzito mkubwa wa magari pamoja na athari za mvua.

115. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande mwengine, Afisi Kuu Pemba imefanya ufuatiliaji wa miradi na kubaini kuwa Miradi ya Maji inaendelea kutoa huduma kwa wananchi na katika baadhi ya maeneo ya miradi kazi za ujenzi wa chemba zinaendelea (Tangi la Chanjaani na Kiwani). Aidha, ufuatiliaji na Tathmini umefanyika katika Shehia ya Kengeja Mkoa wa Kusini Pemba, kwa lengo la kutambua sababu zinazopelekea kukosekana kwa huduma ya maji katika Shehia hiyo. Tathmini imebainisha kuwa Shehia ya Kengeja ina vijiji (tisa) ambapo kwa sasa vinakabiliwa na changamoto ya ukosefu wa huduma ya maji kutokana na kuwepo kwa miundombinu ya zamani ambayo yameshachakaa. Vijiji hivyo ni; Kaani, Sokoni, Mjiweni, Likoni, Usiwambini, Mkumbi, Mwakungu, Jovu na Majenzi.

**116. Mheshimiwa Spika,** shughuli za uchukuaji wa maliasili zisizorejesheka katika kware zote zilizopo kisiwani Pemba zimeratibu zinaonekana katika **Kiambatisho Namba 10.**

## 4.0 UTEKELEZAJI WA BAJETI INAYOZINGATIA JINSIA (GRB)

**117. Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Maji, Nishati na Madini inatambua umuhimu wa utekelezaji wa bajeti inayozingatia jinsia (Gender Responsive Budget - GRB) katika kuhakikisha usawa wa kijinsia na maendeleo jumuishi katika sekta za maji, nishati na madini. Wizara inatarajia kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia misingi ya bajeti inayozingatia jinsia na usawa ambayo inalenga kuhakikisha rasilimali zinagawanywa kwa haki ili kukidhi mahitaji ya jamii ikiwemo wanawake, wanaume, vijana na makundi mengine yenye mahitaji maalum. Katika muktadha wa Bajeti Inayozingatia Usawa wa Kijinsia Wizara ya Maji, Nishati na Madini imebainisha maeneo kadhaa ya kipaumbele katika utekelezaji wake wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

**118. Mheshimiwa Spika,** Wizara inalenga kuongeza ushiriki wa wanawake katika sekta ya maji na nishati kwa asilimia 20 hadi 30 ndani ya kipindi cha miaka mitano ijayo. Kama sehemu ya mkakati huu, jumla ya wahitimu wa kike 100 watapewa fursa ya kufanya mafunzo kwa vitendo kwa kipindi cha miezi sita katika Wizara kupitia taasisi na idara zilizomo ndani ya Wizara. Wizara inatarajia kuwa mwishoni mwa utekelezaji wa mradi wa ZESTA, baadhi ya wahitimu waliofanya vizuri wataajiriwa moja kwa moja katika taasisi walizofanya mafunzo, ili kuongeza idadi ya wataalamu wanawake katika ajira za sekta ya nishati.

**119. Mheshimiwa Spika,** Wizara inakusudia kupanua wigo wa utoaji wa huduma za nishati katika maeneo ya vijijini. Serikali italipa kipaumbele suala la mahitaji ya nishati kwa wanawake, hususan kwa matumizi ya nishati safi nyumbani, biashara ndogo ndogo, na huduma muhimu za jamii kama shule na vituo vya afya. Vile vile Wizara mradi wa ZESTA unaofadhiriwa na Banki ya Dunia, itatoa kipaumbele kwa kaya masikini zinazoongozwa na wanawake wa kipato cha chini ili kuhakikisha kaya hizo zinapata huduma za umeme na nishati mbadala kwa kwa urahisi.

**120. Mheshimiwa Spika,** sambamba hilo, WMNM itahakikisha inaandaa Mikakati ya kuwezesha upatikanaji wa nishati safi ya kupikia kwa wakina

mama (Clean Cooking Strategy) ili kuwarahisishia wakina mama katika shughuli zao za kila siku na kupunguza athari zitokanazo na matumizi ya nishati za kuni na mkaa. Kupitia mikakati hiyo, Wizara inatarajia kuwaunga mkono wanawake kwa kuwarahisishia upatikanaji wa vifaa vya nishati safi kama vile majiko bora ya kupikia yanayotumia Gesi asilia (ikiwemo LPG), vifaa vya mifumo ya nishati mbadala kama vile nguvu za jua na vyenginevyo. Hii ni sehemu ya utekelezaji wa Sera mpya ya Nishati ya Mwaka 2025 pamoja na utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Nishati Safi ya Kupikia wa Tanzania wa mwaka 2024 – 2034.

121. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Sekta ya Maji Wizara itawekeza kwenye miradi ya maji na kuwaunganishia maji wananchi majumbani (*household connection*) kwa lengo la kupunguza adha na masafa ya kutafuta maji umbali mrefu, hasa kwa wanawake na wasichana. Hii itahusisha kuendelea na ujenzi wa miundombinu ya maji katika maeneo ya vijijini na mijini pamoja na maeneo ya jamii jirani na kuwafikishia huduma hizo karibu na maeneo wanayoishi. Kadhalika Wizara inakusudia kuimarisha ukusanyaji wa takwimu zenye kuzingatia mgawanyo wa kijinsia kwa kuweka mkazo ukusanyaji wa takwimu hizo ili kuwezesha upangaji bora wa rasilimali na kufuatilia athari za maamuzi ya bajeti katika jamii. Muhtasari wa takwimu *(Statistical Abstract)* utachapishwa kila mwaka ili kusaidia serikali kuelekeza mikakati zaidi kwenye maeneo yanayohitaji msaada mkubwa.

122. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imepanga kuendelea na kutoa mafunzo ya muda mfupi na mrefu kwa watumishi wa kike ili kuziba pengo la wataalamu wa kike katika fani za kiufundi na kiuhandisi ikiwemo uhandisi na ufundi wa maji, jiolojia ya maji, uhandisi wa umeme na uhandisi wa mafuta na gesi. Vilevile, Wizara itatoa mafunzo ya kujenga uelewa na warsha kwa watumishi wa Wizara kuhusu ujumuishaji wa kijinsia katika maamuzi pamoja na athari za ukatili wa kijinsia (GBV) katika sehemu za kazi. Mambo hayo yataenda sambamba na ufanyaji wa utafiti maalumu unaohusu nafasi na ushiriki wa wanawake katika maendeleo ya sekta ya nishati na madhara chanya ya kiuchumi yanayotokana na ushiriki wao.

123. **Mheshimiwa Spika,** Kwa kuzingatia utekelezaji wa mikakati hii, Wizara ya Maji, Nishati na Madini imetenga kiasi cha fedha **TZS. Milioni 362,960,000** katika bajeti ya mwaka wa fedha 2025/2026 chini ya mpango

wa Bajeti inayozingatia usawa wa kijinsia. Lengo ni kuhakikisha kuwa mipango na mikakati ya Wizara inawanufaisha wananchi wote kwa usawa, hivyo kuchochea maendeleo ya kijamii na kiuchumi nchini kote.

## 5.0 UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO

124. **Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Maji Zanzibar kwa kipindi cha Julai-Machi, 2025 imepanga kukusanya na kutumia **TZS. 110,069,012,415** kwa kazi za ujenzi wa miradi ya maendeleo. Hadi Machi, 2025 jumla **TZS. 26,719,260,615** zimetumika sawa na asilimia **24** ya makadirio. Utekelezaji wa miradi ya maendeleo ni ufuatao: -

### 5.1 Mradi wa Uhuishaji na Uimarishaji wa Mfumo wa Usambazaji Maji Zanzibar - Exim 92.18 mil. USD

125. **Mheshimiwa Spika,** mradi umekamilika na uko katika uangalizi wa mwaka mmoja ili kufuatilia maendeleo ya miundombinu na kutatua hitilafu. Kuanzia Julai hadi Machi 2025, mradi umepangiwa **TZS. 27,438,714,000,** ambapo **TZS. 10,154,964,000** ni kutoka Serikalini kwa fidia za wananchi na **TZS. 17,283,750,000** kutoka kwa Muhisani kwa malipo ya wakandarasi. Hadi Machi 2025, hakuna fedha zilizopatikana kutoka Serikalini na **TZS. 20,283,412,517** zimepatikana kutoka kwa Muhisani.

### 5.2 Programu ya Uimarishaji wa Miundombinu ya Maji Zanzibar

126. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii ina lengo la kuimarisha Miundombinu ya Maji Unguja na Pemba ili kuifanya huduma kuwa toshelevu na endelevu. Kwa kipindi cha Julai - Machi, 2025 Mamlaka imepanga kutekeleza kazi zinazoonekana katika **Kiambatisho Namba 11.**

### 5.3 Mradi wa Uimarishaji wa Huduma za Usambazaji Maji na Miundombinu ya Maji Mjini - (JICA)

127. **Mheshimiwa Spika,** Mradi huu una lengo la kuimarisha miundombinu ya maji Mkoa wa Mjini Magharibi. Aidha, kwa kipindi cha Julai - Machi, 2025 Mradi ulipangiwa kutumia **TZS. 2,531,752,577** kwa ajili ya malipo ya Mshauri Elekezi. Hadi Machi, 2025 jumla ya **TZS. 858,966,184.79** sawa na asilimia **34** ya makadirio zimetumika.

## 5.4 Programu ya UNICEF

128. **Mheshimiwa Spika**, programu hii inatekelezwa na Mamlaka ya Maji Zanzibar kwa ushirikiano na UNICEF, ikilenga kutambua visima binafsi na kutibu maji. Kuanzia Julai hadi Machi 2025, programu ilipangiwa kutumia **TZS. 40,000,000**. Hadi Machi, 2025 **TZS. 81,414,350** zimepatikana na kutumika kununua dawa ya kutibu maji.

## 4.5 Mradi wa Uimarishaji Miundombinu ya Maji – (Kfw)

129. **Mheshimiwa Spika,** Mradi huu unatekelezwa kwa ushirikiano kati ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Benki ya Maendeleo ya Ujerumani (KfW). Mradi utatumia Euro 25 milioni kwa ajili ya kuimarisha miundombinu ya maji Pemba. Hadi Machi 2025, mradi ulipangiwa kutumia **TZS. 51,445,945,867** kwa ajili ya malipo ya Mshauri Elekezi na Mkandarasi. Hadi Machi, 2025 hakuna fedha zilizopatikana kupitia mradi huu.

## 4.6 Mradi wa Usalama wa Maji na Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi Mijini (GiZ)

130. **Mheshimiwa Spika,** Mradi huu unalenga kuimarisha sekta ya maji nchini kwa kusaidia Wizara ya Maji, Nishati na Madini katika usimamizi wa mikakati, kuanzisha mfumo wa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, na kuijengea uwezo Mamlaka ya Maji Zanzibar. Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, mradi umepangiwa **TZS. 2.67 bilioni** kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Shughuli zilizotekelezwa kati ya Julai - Machi 2024/2025 zinaonekana katika **Kiambatisho Namba 12.**

## 4.7 Mradi wa Mabadiliko ya Sekta ya Nishati na Upatikanaji wa Huduma ya Umeme Zanzibar (ZESTA)

131. **Mheshimiwa Spika,** Mradi huu ni mkopo kutoka Benki ya Dunia wenye thamani ya jumla ya Dola za Marekani milioni 142 kwa lengo la kuimarisha sekta ya nishati na upatikanaji wa huduma ya umeme Zanzibar. Mradi unatekelezwa na Wizara ya Maji, Nishati na Madini na Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO). Katika kipindi cha Julai – Machi, 2024/2025 mradi umetumia jumla ya **TZS. 1,826,120,082.25** kwa upande wa Wizara na **TZS. 38,576,601,000** kwa upande wa ZECO na kutekeleza shughuli zifuatazo:-

### 4.7.1 Uendelezaji wa uzalishaji umeme kwa kutumia nishati jadidifu ya jua (solar pv) na miundombinu ya kuhifadhia umeme (Battery Energy Strage System, BESS)

132. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO) linaendelea na taratibu za manunuzi kama ifuatavyo: -

**a) Mkandarasi wa ufungaji wa kituo cha kufua umeme wa nishati jadidifu ya jua**

133. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia Shirika la Umeme imekamilisha tathmini ya zabuni ya mkandarasi wa ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme wa nishati jadidifu ya jua chenye uwezo wa Megawati 18 Makunduchi. Ripoti ya tathmini imewasilishwa Benki ya Dunia kuomba kibali ili kampuni zilizopita katika tathmini ya awali zifunguliwe nyaraka zao za fedha na Mkataba wa mkandarasi kusainiwa Juni, 2025.

134. **Mheshimiwa Spika,** aidha, Kampuni ya Potential Ltd inaendelea na kazi ya ujenzi wa uzio katika eneo la Makunduchi kwa ajili ya uwekaji wa miundombinu ya kuzalishia umeme wa jua ambapo ujenzi wa uzio huo umefikia asilimia **80** na Mkandarasi anatarajia kukabidhi kazi yote mwisho wa mwaka huu wa fedha.

**b) Ufungaji wa kihifadhio (BESS) katika eneo la Mtoni**

135. Mheshimiwa Spika, Vile vile, Shirika la Umeme Zanzibar linaendelea kufanya tathmini ya kitaalamu ya kumpata Mkandarasi wa uwekaji wa mitambo ya kuhifadhi umeme wa jua (*Battery Energy storage infrastructure, BESS*). Mkataba wa kumpata Mkandarasi huyo unatarajiwa kusainiwa mwisho wa mwaka huu wa fedha baada ya taratibu zote kukamilika kulingana na taratibu za Banki ya Dunia.

### 4.7.2 Uimarishaji wa njia za kusafirisha na kusambaza umeme Unguja na vituo vya kupozea na kutawanya umeme

136. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia ZECO kwa kushirikiana na Mkandarasi JOINT VENTURE OF ZTT (CHINA) AND JONGRO (SOUTH KOREA) imekamilisha kazi za "geotechnical investigation" kwenye nguzo za kona pamoja na upimaji wa njia yote ya ukubwa wa kilomota 100. Mkandarasi anaedelea na kazi ya *"geotechnical investigation"* kwa ajili ya maeneo zitakazojengwa *"towers"* (*suspension towers locations*) pamoja na usanifu

wa njia ya umeme. Kwa upande wa ujenzi wa vituo vitatu vya kupoozea umeme, Mkandarasi SIEYUAN ELECTRIC CO LTD YA KUTOKA CHINA amekamilisha kazi ya kusafisha maeneo yote ya ujenzi wa vituo na anaendelea na ujazaji wa udongo katika vituo vyote vitatu viliopo Welezo, Matemwe na Makunduchi.

### 4.7.3 Ujenzi wa kituo cha uendeshaji (Supervision Control and Data Acquisition - SCADA) wa mifumo ya umeme kwa ajili ya misongo ya umeme ya kilovoti 132, 33 na 11

137. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia ZECO umekamilisha ripoti ya tathmini ya kitaalamu kwa ajili ya kumpata Mkandarasi wa uwekaji wa mfumo huo, ripoti hiyo imeshatolewa ridhaa na Benki ya Dunia. Aidha, ZECO imeshakamilisha tahmini ya kifedha na kuwasilisha ripoti hiyo kwa Benki ya Dunia kwa ajili ya kupatiwa ridhaa. Mkandarasi atakayeshinda zabuni hiyo anatarajiwa kusaini Mkataba mwisho wa mwezi wa Juni 2025.

### 4.7.4 Uboreshaji wa njia za usambazaji umeme Mji Mkongwe (Stone town), uendelezaji wa njia mpya (extension) za misongo ya kilovoti 33 na 11 katika visiwa vya Unguja na Pemba

138. **Mheshimiwa Spika**, Wizara kupitia ZECO kwa kushirikiana na Mshauri Elekezi imekamilisha uandaaji wa nyaraka tatu (3) ya zabuni kwa ajili ya kutangaza zabuni ya kuwapata wakandarasi watatu (3) wa uboreshaji wa njia za usambazaji umeme. Nyaraka zilizokamilika kutangazwa na kufunguliwa kwa zabuni ni; zabuni ya Mji Mkongwe, Zabuni ya Kisiwa cha Unguja na Zabuni ya Kisiwa cha Pemba. Aidha, mchakato wa kupitia nyaraka za wazabuni umeshanza kuwatafuta wakandarasi wa ujenzi wa usambazaji umeme Mji Mkongwe na uendelezaji wa njia mpya za misongo ya kilovolti 33 na 11 kwa Unguja na Pemba unaendelea na inakusudiwa kukamilika ndani ya mwaka 2025 kwa kutiwa saini na wakandarasi watakaopatikana.

### 4.7.5 Uunganishaji wa mifumo ya utayarishaji wa bili za malipo kwa ZECO (SAP ERP and Hexing AMR Billing System Integration and Customer Data Migration)

139. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia ZECO imekamilisha kutengeneza nyaraka za miongozo (*Standard Operating Procedure, SOP*) pamoja na kuandaa nyaraka za mahitaji ya mtumiaji *"User Requirement"* kwenye

SAP na Hexing. Kampuni inaendelea kufanya mapitio ya nyaraka kwa ajili ya utekelezaji wa kazi hizo. ZECO inatarajia kusaini mkataba wa muda mfupi na Kampuni ya HEXING ya China kwa ajili ya kukamilisha taarifa za mifumo ya bili za wateja.

### 4.7.6 Tathmini ya Fidia kwa waathirika (Resettlement Action Plan) na Mazingira (Environmental and Social Impact Assessment (ESIA) na Fidia

140. **Mheshimiwa Spika,** Wizara inaendelea na zoezi la ulipaji fidia kwa waathirika wa mradi ZESTA katika maeneo ya mradi ambapo asilimia 95 ya waathirika wa mradi tayari wameshalipwa fidia pamoja na kupewa barua za kuwataka kuondoka katika maeneo hayo ili kupisha shuhuli za ujenzi. Zoezi la ulipaji fidia linaendelea, hata hivyo kumekua na changamoto ya upatikanaji wa taarifa za kibenki kwa baadhi ya waathirika wa mradi na ambao hawajalipwa.

141. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kwa kushirikiana na Mshauri Elekezi imekamilisha kuandaa rasimu ya ripoti ya mwisho (*final draft report*) ya makisio ya matumizi ya umeme (*demand forecasting*) kwa kipindi cha miaka 20. Rasimu hiyo tayari imesharidhiwa na Benki ya Dunia. Pamoja na hilo, mradi umekamilisha ripoti ya mpango wa vyanzo vya kuzalishia umeme. Mshauri elekezi anaendelea kukamilisha ripoti ya mwisho ya kuanisha vyanzo vya kuzalisha umeme kwa gharama nafuu (*Least Cost generation option report*). Ripoti hiyo inatarajiwa kukamilika mwisho wa mwaka huu wa fedha.

### 4.7.7 Kazi ya ushauri elekezi ya Tathmini na kuandaa mpango wa ujuzi na mahitaji katika sekta ya Nishati (Sector skills and capacity need assessment)

142. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kwa kushirikiana na Mshauri Elekezi imekamilisha kuandaa ripoti zote kwa mujibu wa matakwa ya mkataba. Mkataba huo umefikia kikomo Machi, 2025 na mshauri elekezi amekabidhi nyaraka zote zinazohitajika.

**4.7.8 Kazi ya ushauri elekezi ya kuandaa Mfumo wa Kisheria, Kitaasisi, Kikanuni na Mikataba kwa Maendeleo ya Nishati Mbadala. (Consultant Services for legal, institutional, regulatory and contractual framework for Renewable Energy Development)**

143. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kwa kushirikiana na Mshauri Elekezi imekamilisha uandaaji wa rasimu ripoti ya kubainisha mapungufu ya kikanuni na kisheria (*Gap analaysis report: Task 1*) pamoja na kukamilisha rasimu ya kubainisha viashiria hatarishi (*Risk allocation mtrix: Task 2*). Rasimu hizo zimewasilishwa Benki ya Dunia kwa ajili ya kutolewa maoni na kupatiwa ridhaa.

**4.7.9 Kazi ya ushauri elekezi ya kwa Shirika lisilo la Kiserikali la Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa RAP (Consultancy services for RAP implementation monitoring NGO)**

144. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kwa kushirikiana na kampuni ya ENVICON inaendelea na zoezi la ufatiliaji wa ulipaji fidia na kuhakikisha taratibu zote zinafuatwa bila ya malalamiko ambapo Kampuni hiyo kwa asilimia 85 imekamilisha zoezi la kutembelea maeneo ya mradi na waathirika wake. Aidha, mradi umekamilisha kuandaa ripoti ya robo mwaka (Januari-Machi, 2024/2025) ya ufuatiliaji wa utekelezaji wa zoezi la ulipaji fidia. Ripoti hiyo tayari imeshaidhinishwa na Benki ya Dunia.

145. **Mheshimiwa Spika,** Wizara inaendelea kukamilisha taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mshauri Elekezi wa kuandaa Sheria ya Nishati na Kanza data ya Nishati.

**4.8 Mradi wa Uboreshaji wa Mfumo wa Umeme Zanzibar**

146. **Mheshimiwa Spika,** Wizara, kupitia Kampuni ya Novavis ipo katika hatua za mwisho za kukamilisha mradi wa kuboresha mfumo wa umeme Zanzibar, ambapo tayari ufungaji wa Voltage Regulator katika maeneo 11 (8 Unguja na 3 Pemba) na Capacitor Bank katika maeneo 31 (26 Unguja na 5 Pemba) umekamilika kwa sasa usakinishaji STATCOM katika eneo la Mtoni Unguja unaendelea na unategemewa kukamilika mwisho wa mwaka wa fedha 2024/2025.

147. **Mheshimiwa Spika,** Mradi huu unalenga kuboresha kiwango (voltage) cha upatikanaji, usambazaji umeme kwenye mondo wa (33 kV na 11 kV)

na kutatua changamoto ya umeme mdogo, isipokuwa katika eneo la Ubago na maeneo ya Wesha, Pujini dodo na Kiungoni Pemba. Kukamilika kwa kifaa hiki kutahakikisha voltage ya umeme kutoka Tanzania Bara inakuwa thabiti na ya kutosha.

## 6.0 MWELEKEO WA BAJETI YA WIZARA YA MAJI, NISHATI NA MADINI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

148. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Maji, Nishati na Madini kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 itatekeleza bajeti yake kwa kuzingatia vipaumbele vifuatavyo: -

i. Kushirikisha Wawekezaji binafsi katika kuimarisha upatikanaji wa huduma tunazozitoa (Maji, Nishati na Madini);

ii. Kuimarisha Nyenzo na kuboresha uwezo wa Taasisi katika kudhibiti huduma za Maji na Nishati;

iii. Kuimarisha hali ya usambazaji na upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama, Nishati na Madini;

iv. Kuendelea kufanya tafiti kwa lengo la kuimarisha upatikanaji wa huduma zinazotolewa na sekta zilizo chini ya Wizara na

v. Kutekeleza na kusimamia miradi mikubwa ya Kimkakati.

149. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Maji, Nishati na Madini itatekeleza vipaumbele hivyo kupitia Programu Kuu tatu (3) na Programu Ndogo sita (6) zifuatazo: -

### A. Programu Kuu PN0301: Usimamizi wa Huduma za Maji

Programu hii itatekelezwa kupitia Programu Ndogo moja (1) ambayo ni;

i. Usimamizi na Uratibu wa Huduma za Maji.

150. **Mheshimiwa Spika,** Katika kufikia malengo ya Programu hii, Wizara kupitia Idara ya Maendeleo ya Maji itatekeleza shughuli zifuatazo: -

i. Kusimamia utekelezaji wa shughuli za usambazaji wa maji safi na usimamizi wa usafi wa mazingira (maji taka) kwa wote;

ii. Kuhifadhi na kusimamia rasilimali maji Unguja na Pemba;

iii. Kuanzisha na kusimamia mfumo wa taarifa za ubora na wingi wa rasilimali maji Unguja na Pemba;

iv. Kuandaa miongozo ya uendelezaji wa rasilimali maji na usafi wa mazingira;

v. Kuandaa tafiti mbalimbali za vyanzo vya maji katika sekta ya maji safi na maji taka;

vi. Kuandaa mfumo wa utoaji vibali na leseni ya uendelezaji rasilimali maji na maji taka na

vii. Kuanzisha jumuia shirikishi za uhifadhi maji katika shehia na kuwajengea uwezo juu ya uhifadhi na usimamizi wa rasilimali maji.

151. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii itaenda sambamba na utekelezaji unaofanywa na Kampuni ya "RAND WATER ZANZIBAR" inayotekeleza shughuli za ZAWA kwa sasa. Hivyo, Kampuni hiyo itatekeleza shughuli zifuatazo: -

i. Kusimamia, kuboresha na kuiendesha miundombinu ya Maji kwa kuwaunganishia wananchi.

ii. Kufanya uwekezaji wa teknolojia na miundombinu ya kusambazia maji

iii. Kukusanya mapato kutokana na utoaji huduma ya maji

iv. Kuwajengea uwezo watendaji pamoja na Kuzijengea uwezo Ofisi za wilaya

v. Kukusanya mapato kutokana na utoaji huduma ya maji

vi. Kuwekeza katika miradi mipya ya maji na kuimarisha miundombinu iliyopo

152. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 Kampuni ya RAND WATER ZANZIBAR inatarajia kukusanya jumla ya **TZS. 13,289,000,000.00** kupitia vyanzo vyake vya mapato ambavyo ni; mauzo ya maji, mapato ya huduma nyenginezo, na ruzuku ya mshahara ya wafanyakazi wa ZAWA.

Aidha, Kampuni imekadiria kutumia jumla ya **TZS. 13,289,000,000.00** kwa ajili ya utekelezaji wa kazi za kawaida na uendeshaji.

153. **Mheshimiwa Spika,** ili Programu Kuu ya Usimamizi wa Huduma za Maji iweze kutekelezeka kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, naliomba Baraza Lako Tukufu kuidhinisha jumla ya **TZS. 165,518,634,000** kwa ajili ya matumizi mengineyo, mishahara, ruzuku ya mishahara na kazi za miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, **TZS. 543,010,000** kwa ajili ya matumizi mengineyo, **TZS. 307,435,000** kwa ajili ya mishahara, **TZS. 10,110,400,000** kwa ajili ya ruzuku ya mishahara na **TZS. 154,557,789,000** kwa ajili ya kazi za miradi ya maendeleo.

**B. Programu Kuu PN0302: Usimamizi wa Huduma za Nishati na Madini**

Programu hii itatekelezwa kupitia Programu Ndogo mbili ambazo ni: -

i. Programu Ndogo ya Usimamizi na Uimarishaji wa Huduma za Nishati na

ii. Programu Ndogo ya Usimamizi na Uimarishaji wa Huduma za Madini.

154. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii itatekelezwa kupitia Idara ya Nishati na Madini na ikihusisha utekelezaji wa shughuli za Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA) na Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO). Kupitia Idara ya Nishati na Madini Programu hii itatekeleza shughuli zifuatazo: -

i. Kutoa elimu ya matumizi ya Nishati Mbadala, Nishati Sanifu na Nishati za Kisasa kwa Jamii Hususan Wanawake;

ii. Kusimamia utekelezaji wa Sera ya Nishati ya Mwaka 2025;

iii. Kufanya tafiti za vyanzo tofauti vya nishati;

iv. Kusimamia Ufuatiliaji wa Miradi ya Nishati na

v. Utoaji wa elimu kwa wananchi juu ya upatikanaji wa maliasili zisizorejesheka.

155. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO) kupitia Programu hii itetekeleza shughuli zifuatazo: -

i. Kupeleka umeme Vijijini na Mashambani;

ii. Kuongeza idadi ya wateja wapya;

iii. Kuondosha tatizo la umeme mdogo kwa maeneo ambayo yamezidiwa; na

iv. Kuongeza ukusanyaji wa mapato kwa kuwafungia wateja *pre-paid smart meter*.

156. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO) linatarajia kukusanya jumla ya **TZS. 265,326,593,941.00** kupitia vyanzo vyake vya mapato ambavyo ni; mauzo ya umeme, mapato ya huduma nyenginezo, mchango wa Serikali na makusanyo ya madeni ya nyuma ya wateja. Shirika limekadiria kutumia jumla ya **TZS. 265,262,155,475.00** kwa ajili ya utekelezaji wa kazi za kawaida na kazi za maendeleo. Aidha, ifikapo tarehe 30 Juni, 2026 Shirika linatarajia kupata bakaa ya jumla ya **TZS. 64,438,466.00.**

157. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA) kupitia programu hii imejipangia kutekeleza shughuli zifuatazo: -

i. Kuimarisha Nyenzo za Udhibiti wa huduma za Maji na Nishati;

ii. Kuimarisha upatikanaji bora, endelevu na salama wa huduma za maji na nishati;

iii. Kuimarisha mazingira ya kazi na maslahi ya wafanyakazi;

iv. Kuboresha uwezo wa Taasisi wa kudhibiti Huduma za Maji na Nishati na

v. Kutoa elimu pamoja na kuongeza uelewa kwa umma kuhusu Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati.

158. Mheshimiwa Spika, kwa Mwaka wa Fedha, 2025/2026 ZURA imejipangia kukusanya jumla ya **TZS. 31,164,000,000** kutokana na tozo la Mamlaka **"Regulatory Levy"** inayotokana na mafuta, gesi ya kupikia (LPG) mapato ya leseni na mapato mengineyo. Aidha, imekadiria kutumia jumla ya **TZS. 31,164,000,000** kwa ajili ya kazi za kawaida, Maendeleo na Mchango wa

Mfuko Mkuu wa Serikali. Kati ya fedha hizo, **TZS. 6,434,000,000** kwa ajili ya kazi za kawaida, **TZS. 4,500,000,000** kwa ajili ya Mishahara, **TZS. 10,230,000,000** kwa ajili ya kazi za Maendeleo na **TZS. 10,000,000,000** kwa ajili ya Mchango wa Mamlaka katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

**159. Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 Wizara kutokana na Maliasili zisizorejesheka, imepangiwa kukusanya jumla ya **TZS. 20,750,419,000.** Makusanyo hayo yanatokana na maombi ya vibali, ada, leseni na faini zitokanazo na malipo ya Maliasili hizo.

**160. Mheshimiwa Spika,** ili Programu Kuu ya Usimamizi wa Huduma za Nishati na Madini iweze kutekelezeka kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya **TZS. 52,004,874,000** kwa ajili ya matumizi mengineyo, mishahara na kazi za maendeleo. Kati ya fedha hizo, **TZS. 316,783,000** kwa ajili ya matumizi mengineyo, **TZS. 889,116,000** kwa ajili ya mishahara na **TZS. 50,798,975, 000** kwa ajili ya kazi za maendeleo.

## C. Programu Kuu PN0303: Uendeshaji na Uratibu wa Mipango ya WMNM

Programu hii itatekelezwa kupitia Programu Ndogo tatu ambazo ni: -

i. Programu Ndogo ya Utawala na Uendeshaji wa WMNM;

ii. Programu Ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Utafiti wa WMNM; na

iii. Programu Ndogo ya Uratibu na Utekelezaji wa shughuli za WMNM-Afisi Kuu Pemba.

**161. Mheshimiwa Spika,** Programu hii imejipangia kutekeleza shughuli zifuatazo: -

i. Kutoa huduma za uendeshaji wa Ofisi katika Wizara ya Maji Nishati na Madini;

ii. Kuwajengea uwezo wafanyakazi kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu, muda mfupi na ya ndani;

iii. Kuandaa, Kusimamia na Kufanya Mapitio ya Sera, Sheria, Kanuni na Miongozo yake.

iv. Kufuatilia na Kufanya Tathmini ya Utekelezaji wa Sera za WMNM.

v. Kukusanya na kuchambua takwimu za utekelezaji wa Shughuli za WMNM zilizoainishwa kijinsia na

vi. Kuratibu na kukuza mashirikiano ya kisekta na usimamizi wa utekelezaji wa shughuli za Wizara.

162. **Mheshimiwa Spika,** ili Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Mipango ya Wizara iweze kutekelezeka kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya **TZS. 3,302,256,000** kwa matumizi ya kazi za kawada na mishahara. Kati ya fedha hizo, **TZS. 1,578,207,000** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **TZS. 1,724,049,000** kwa ajili ya mishahara.

## 7.0 MAOMBI YA FEDHA KWA KAZI ZILIZOPANGWA KUTEKELEZWA KATIKA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

163. **Mheshimiwa Spika,** ili kuiwezesha Wizara ya Maji, Nishati na Madini kutekeleza Programu zake na kazi zilizopangwa kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, naliomba Baraza lako kuidhinisha makadirio ya matumizi ya Programu za Wizara kwa Fungu N03 lenye jumla ya **TZS. 220,825,764,000** kwa ajili ya matumizi mengineyo, mishahara, ruzuku ya mishahara na miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, **TZS. 2,438,000,000** kwa ajili ya matumizi mengineyo, **TZS. 2,920,600,000** kwa ajili ya mishahara, **TZS. 10,110,400,000** kwa ajili ya ruzuku ya mishahara, **TZS. 205,356,764,000** kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Mgawanyo wa fedha zitakazotumika kwa utekelezaji wa kila Programu umeainishwa katika **Kimbatisho Namba. 13.**

Vile vile, naomba idhini ya kukusanya **TZS. 20,750,419,000** kutoka katika vyanzo mbali mbali vya mapato yatokanayo na maliasili zisizorejesheka.

## 8.0 HITIMISHO

164. **Mheshimiwa Spika**, naomba nichukue fursa hii kwa mara nyengine kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa namna anavyotekeleza kwa ufanisi Dira ya Maendeleo ya Zanzibar 2020-2050 pamoja na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020-2025 kwa vitendo.

165. **Mheshimiwa Spika,** tunashuhudia mabadiliko makubwa ya kiutendaji na ya kisasa kupitia miradi mbali mbali ya kimkakati ndani ya kipindi kifupi tu cha uongozi wake. Kwa kweli hakuna alilobakisha katika mipango yetu na ameitekeleza Ilani ya Chama chetu kwa zaidi ya asilimia 100. Niwasihi Waheshimiwa Wawakilishi wenzangu tuungane na Mheshimiwa Rais wetu mpendwa ili kuhakikisha Chama cha Mapinduzi kinaendelea kushika usukani na kuendelea kuwaletea maendeleo wananchi.

166. **Mheshimiwa Spika,** naomba kuwapongeza kwa dhati wale wote tulioshirikiana nao katika maandalizi ya Hotuba hii akiwemo Naibu Waziri Mheshimiwa Zawadi Amour Nasor, Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Nishati na Madini Ndugu Joseph John Kilangi, Naibu Katibu Mkuu Ndugu Mwanajuma Majid Abdullah, Wakurugenzi Wakuu wa Taasisi, Wakurugenzi wa Idara za Wizara pamoja na wafanyakazi wote wa Wizara na Taasisi zilizochini ya Wizara yetu.

167. **Mheshimiwa Spika,** kwa hakika tumekua tukishirikiana vyema kwa takriban miaka minne sasa, uzalendo na uchapaji kazi wao mkubwa umesaidia kuweza kuzitatua kwa pamoja changamoto za ukosefu wa maji na umeme zinazowakabili wananchi wa Zanzibar.

168. **Mheshimiwa Spika,** naomba nichukue nafasi hii kushukuru na kuthamini michango na ushirikiano kutoka kwa washirika na wadau wetu wa maendeleo wa ndani na nje ya nchi wakiwemo Taasisi ya Ufuatiliaji wa Utendaji Serikali (PDB), Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ), Benki ya CRDB, Benki ya NMB, Benki ya Exim ya INDIA, Benki ya Maendeleo ya Ujerumani (KfW), Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Benki ya Dunia (WB), Umoja wa Ulaya (EU), Shirika la Fedha Duniani (IMF), pamoja na Taasisi na Mashirika ya UNICEF,  JICA (Japan), GWPSA na GWPTZ, GiZ (Ujerumani), NEC (Oman), NORAD (Norway), SIDA (Sweden), UNDP, Action Aid, Uongozi Institute na Wadau wengine wa maendeleo.

169. **Mheshimiwa Spika,** nawashukuru Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza lako Tukufu kwa kunisikiliza kwa umakini mkubwa wakati wote wa kuwasilisha Hotuba hii. Kwa heshima kubwa nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu waipokee, waipitie, waijadili na hatimae waipitishe bajeti ya Wizara ya Maji, Nishati na Madini kwa mwaka wa fedha 2025/2026

170. **Mheshimiwa Spika,** shukrani zangu za dhati nizitoe tena kwa wananchi wangu wa Jimbo la Chake Chake ambao kwa muda wote wameendelea kuniamini na kuniunga mkono katika kuimarisha maendeleo ya Jimbo na Taifa kwa ujumla. Pia, nawashukuru kwa ushirikiano wanaoendelea kunipatia katika kutekeleza majukumu yangu ya Jimbo na Kitaifa na wakati mwingine kunivumilia kwa kukosa huduma yangu ninapokuwa nikitekeleza majukumu ya kitaifa. Niwaahidi ya kwamba nitaendelea kuwa pamoja nao na kuwahakikishia kuwa nitawatumikia kwa moyo wangu wote kadri Mwenyezi Mungu atakavyonijalia ili kuchochea Maendeleo ya Jimbo na Taifa letu.

171. **Mheshimiwa Spika,** mwisho japo si kwa umuhimu, naomba sasa nichukue fursa hii adhimu kuishukuru kwa dhati familia yangu, ndugu, jamaa na marafiki zangu pamoja na watoto wangu wote kwa uvumilivu wao na kuniunga mkono pamoja na kuniombea mema kwa Mwenyezi Mungu, ili niweze kutekeleza majukumu yangu kwa ufanisi.

172. **Mheshimiwa Spika,** Baada ya shukrani hizo, sasa nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu waipokee, waijadili, kutushauri na hatimae waipitishe Bajeti hii

173. **Mheshimiwa Spika,** kwa heshima naomba kutoa hoja.

**(Mheshimiwa Shaib Hassan Kaduara)**
**Waziri wa Maji, Nishati na Madini**
**Zanzibar.**

# VIAMBATANISHO

## Kiambatisho Namba. 1: Mapitio ya Upatikanaji wa Fedha kwa Mwaka wa Fedha2024/2025

| PROGRAMU KUU | PROGRAMU NDOGO | TAASISI | MATUMIZI | BAJETI ILIYOPANGWA HADI MACHI, 2025 "000" | | | FEDHA ZILIZOPATIKANA HADI MACHI, 2025 "000" | | | % YA FEDHA ZILIZOPATIKANAKWA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | SMZ | WAHISANI | JUMLA | SMZ | WAHISANI | JUMLA | |
| Usimamizi wa huduma za Maji | Kusimamia Huduma na Upatikanaji wa Maji Safi na Salama | Idara ya Maendeleo ya Maji | Fedha za Matumizi Mengineyo | 550,520,000.00 | | 550,520,000.00 | 151,379,077.04 | | 151,379,077.04 | 27.50 |
| | | | Fedha za Mishahara | 294,214,000.00 | | 294,214,000.00 | 267,069,774.00 | | 267,069,774.00 | 90.77 |
| | | | Ruzuku ya Mshahara | 9,134,300,000.00 | | 9,134,300,000.00 | 6,475,377,977.57 | | 6,475,377,977.57 | 70.89 |
| | | | **Jumla Ndogo** | **9,979,034,000.00** | **-** | **9,979,034,000.00** | **6,893,826,828.61** | **-** | **6,893,826,828.61** | **69.08** |
| | Kuimarisha huduma za Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) | Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) | Fedha za Miradi ya Maendeleo | 154,627,944,549.00 | | 154,627,944,549.00 | 11,593,137,515.45 | 20,036,819,304.48 | 31,629,956,819.93 | 20.46 |
| | | | **Jumla Ndogo** | **164,606,978,549.00** | **-** | **164,606,978,549.00** | **18,486,964,344.06** | **20,036,819,304.48** | **38,523,783,648.54** | **23.40** |
| | **Jumla ya Programu Kuu 1** | | | **164,606,978,549.00** | **-** | **164,606,978,549.00** | **18,486,964,344.06** | **20,036,819,304.48** | **38,523,783,648.54** | **23.40** |
| Usimamizi wa huduma za Nishati na Madini | Usimamizi na Uimarishaji wa Huduma za Nishati | Idara ya Nishati na Madini | Fedha za Matumizi Mengineyo | 251,401,000.00 | | 251,401,000.00 | 201,289,737.00 | | 201,289,737.00 | 80.07 |
| | | | Fedha za Mishahara | 850,880,000.00 | | 850,880,000.00 | 568,696,085.00 | | 568,696,085.00 | 66.84 |
| | | | Fedha za Miradi ya Maendeleo | | | - | | 1,826,120,082.25 | 1,826,120,082.25 | - |
| | | Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO) | Fedha za Miradi ya Maendeleo | 37,255,868,970.00 | 174,000,000,000.00 | 211,255,868,970.00 | 13,416,961,750.00 | 40,382,814,000.00 | 53,799,775,750.00 | 25.47 |
| | | | **Jumla Ndogo** | **38,358,149,970.00** | **174,000,000,000.00** | **212,358,149,970.00** | **14,186,947,572.00** | **42,208,934,082.25** | **56,395,881,654.25** | **26.56** |
| | **Jumla ya Programu Kuu 2** | | | **38,358,149,970.00** | **174,000,000,000.00** | **212,358,149,970.00** | **14,186,947,572.00** | **42,208,934,082.25** | **56,395,881,654.25** | **26.56** |
| Uendeshaji na Uratibu wa Mipango ya WMNM | Utawala na Uendeshaji wa WMNM | Utumishi na Uendeshaji | Fedha za Matumizi Mengineyo | 451,518,000.00 | | 451,518,000.00 | 316,541,199.00 | | 316,541,199.00 | 70.11 |
| | | | Fedha za Mishahara | 758,354,000.00 | | 758,354,000.00 | 667,915,621.00 | | 667,915,621.00 | 88.07 |
| | | | **Jumla Ndogo** | **1,209,872,000.00** | **-** | **1,209,872,000.00** | **984,456,820.00** | **-** | **984,456,820.00** | **81.37** |
| | Uratibu wa Mipango, Sera na Utafiti | Idara ya Mipango, Sera na Utafiti | Fedha za Matumizi Mengineyo | 320,183,000.00 | | 320,183,000.00 | 159,753,689.75 | | 159,753,689.75 | 49.89 |
| | | | Fedha za Mishahara | 149,490,000.00 | | 149,490,000.00 | 133,000,862.00 | | 133,000,862.00 | 88.97 |
| | | | **Jumla Ndogo** | **469,673,000.00** | **-** | **469,673,000.00** | **292,754,551.75** | **-** | **292,754,551.75** | **62.33** |
| | Uratbu wa Utekelezaji wa Shughuli za WMNM - Pemba | Afisi Kuu - Pemba | Fedha za Matumizi Mengineyo | 245,135,000.00 | | 245,135,000.00 | 248,135,850.00 | | 248,135,850.00 | 101.22 |
| | | | Fedha za Mishahara | 547,733,500.00 | | 547,733,500.00 | 269,374,394.00 | | 269,374,394.00 | 49.18 |
| | | | **Jumla Ndogo** | **792,868,500.00** | **-** | **792,868,500.00** | **517,510,244.00** | **-** | **517,510,244.00** | **65.27** |
| | **Jumla ya Programu Kuu 3** | | | **2,472,413,500.00** | **-** | **2,472,413,500.00** | **1,794,721,615.75** | **-** | **1,794,721,615.75** | **72.59** |
| **PROGRAMU KUU** | **PROGRAMU NDOGO** | **TAASISI** | **MATUMIZI** | **BAJETI ILIYOPANGWA HADI MACHI, 2025 "000"** | | | **FEDHA ZILIZOPATIKANA HADI MACHI, 2025 "000"** | | | **% YA FEDHA ZILIZOPATIKANAKWA** |
| | | | | **SMZ** | **WAHISANI** | **JUMLA** | **SMZ** | **WAHISANI** | **JUMLA** | |
| | **JUMLA YA FUNGU NO3** | | | **205,437,542,019.00** | **174,000,000,000.00** | **379,437,542,019.00** | **34,468,633,531.81** | **62,245,753,386.73** | **96,714,386,918.54** | **25.49** |

***Kiambatisho Namba. 2:Vijiji vilivyopatiwa huduma ya umeme***

| Nam. | UNGUJA | Nam. | PEMBA |
|---|---|---|---|
| 1. | Umbuji | 1. | Tondooni Wambaa |
| 2. | Jumbi Mkorogo | 2. | Mwamba Mkundundani |
| 3. | Mchangani Shamba | 3. | Kangagani |
| 4. | Kiboje Uwangani | 4. | Mwamba Mkuu ndagoni |
| 5. | Kijiji cha Uroa | 5. | Kangani mboga mboga |
| 6. | Makunduchi Kigaeni | 6. | Furaha Mvumoni |
| 7. | Kiboje Kinooni | 7. | Mibrani |
| 8. | Kiboje Mwembeshauri | 8. | Andikoni Wambaa |
| 9. | Mgambo Makadara | | |
| 10. | Mgambo | | |
| 11. | Kizimkazi Mchangamle | | |
| 12. | Kiwengwa Melia | | |
| 13. | Donge Mchangani | | |
| 14. | Bwejuu | | |
| 15. | Nyakurungu | | |
| 16. | Makunduchi kajengwa | | |
| 17. | Mchangani Shamba | | |
| 18. | Ukweta | | |
| 19. | Ndagaa Kitoroni | | |
| 20. | Muyuni | | |
| 21. | Muyuni C | | |
| 22. | Muungoni | | |
| 23. | Mchanga -Mle | | |

***Chanzo: ZECO, 2025***

***Kiambatisho Namba. 3: Maeneo yaliyokuwa na tatizo la umeme mdogo ambayo yameshapelekewa ya huduma za umeme***

| Nam. | Unguja | Nam. | Pemba |
|---|---|---|---|
| 1 | Donge Machinjioni | 1 | Msuka |
| 2 | Maungani | 2 | Limboni kwa Boban |
| 3 | Binguni | 3 | Mtoni -chake |
| 4 | Makunduchi Tasani | 4 | Kitongoni Kijijini |
| 5 | Makunduchi Kigaeni | 5 | Mbuyuni Chake |
| 6 | Mbuzini | 6 | Umangani |
| 7 | Kwerekwe | 7 | Malikindi Mbuyuni |
| 8 | Kwa Mchina | 8 | Kinowe |
| 9 | Ufufuma | 9 | Wawi Mtemani |
| 10 | Umbuji | 10 | Tumbe Kojifa. |
| 11 | Mombasa Changu | | |
| 12 | Mfenesini | | |
| 13 | Fuoni Kibondeni | | |
| 14 | Paje | | |
| 15 | Masingini Tangini | | |
| 16 | Uroa | | |
| 17 | Fuoni Uwandani | | |
| 18 | Kizimkazi Mnarani | | |
| 19 | Kidoti Istiqama | | |
| 20 | Fumba Chaleni | | |
| 21 | Bububu Meli nane | | |
| 22 | Mwakaje | | |
| 23 | Dunga | | |
| 24 | Ufufuma | | |
| 25 | Binguni | | |
| 26 | Kwarara Madina | | |
| 27 | Jumbi Kontena | | |
| 28 | GaraGara | | |
| 29 | Kichaka-Punda | | |

***Chanzo: ZECO, 2025***

***Kiambatisho Namba. 4: Matokeo ya Residual Chlorine kwa skimu zilizokaguliwa***

| RESIDUAL CHLORINE MONITORING | | |
|---|---|---|
| **Jina la kituo** | **Free Chlorine (mg/L)** | **Maelezo (Standard: 0.2-0.5 mg/L)** |
| **Skimu ya Dole** | | |
| Mwanyanya 01 | 0.2 | Inaridhisha |
| Mwanyanya 02 | 0.2 | Inaridhisha |
| Kijichi School | 0.2 | Inaridhisha |
| Kijichi House | 0.2 | Inaridhisha |
| Kizimbani Mndo | 0.3 | Inaridhisha |
| **Skimu ya Kidutani** | | |
| Kwarara | 0.4 | Inaridhisha |
| Kinuni | 0.3 | Inaridhisha |
| Meli 4 Uzi | 0.2 | Inaridhisha |
| **Skimu ya Mfenesini** | | |
| Mfenesini 01 | 0.2 | Inaridhisha |
| Sea Cliff | 0.2 | Inaridhisha |
| Mangapwani | 0.2 | Inaridhisha |
| **Skimu ya Dimani** | | |
| Fumba | 0.2 | Inaridhisha |
| Bweleo | 0.3 | Inaridhisha |
| Dimani | 0.5 | Inaridhisha |
| **Skimu ya Maungani** | | |
| Maungani | 0.3 | Inaridhisha |
| Shakani | 0.2 | Inaridhisha |
| Nyamanzi | 0.3 | Inaridhisha |

***Chanzo: ZURA, 2025***

***Kiambatisho Namba. 5: Matokeo yaliyobainika katika ukaguzi wa vituo vikuu vya Umeme***

| Nam. | Jina la Kituo | Mapungufu yaliyogundulika |
|---|---|---|
| 1 | Kituo cha umeme Fumba. (Kituo cha kupokelea umeme kutoka Tanzania Bara) | • Kukosekana kwa alama za tahadhari.<br>• Kuisha muda wa matumizi kwa vifaa vya kuzimia moto.<br>• Kutokuwepo kwa mpango maalumu wa kufanyia matengenezo ya mtambo wa kupoozea waya. |
| 2 | Kituo cha umeme Mtoni<br><br>(Kituo hichi kinapokea umeme kutoka Fumba) | • Kukosekana kwa kisanduku cha huduma ya kwanza.<br>• Kukosekana kwa kompyuta za kurikodia taarifa (data) ambazo zitapatikana Mtoni moja kwa moja.<br>• Kuwepo kwa uoto wa majani katika eneo la kupelekea umeme la njia ya kusafirishia umeme ya megawati 45. |
| 3 | Kituo cha umeme Mwanyanya | • Kukosekana kwa kisanduku cha huduma ya kwanza.<br>• Kukosekana kwa kompyuta za kurikodia taarifa (data) ambazo zitapatikana Mtoni moja kwa moja. |

| | | |
|---|---|---|
| 4 | Kituo cha umeme Welezo | • Kukosekana kwa kisanduku cha huduma ya kwanza.<br>• Kukosekana kwa kompyuta za kurikodia taarifa (data) ambazo zitapatikana Mtoni moja kwa moja.<br>• Vifaa vya kuzimia moto ni vichache. |
| 5 | Kituo cha umeme Mpendae | • Kukosekana kwa kisanduku cha huduma ya kwanza.<br>• Kukosekana kwa vipoza joto kama vile feni kiyoyozi (Aircondition) au feni za kutolea hewa nzito nje.<br>• Kukosekana kwa kompyuta za kurikodia taarifa (data) ambazo zitapatikana Mtoni moja kwa moja.<br>• Kuongezeka kwa matumizi ambapo hupelekea transfoma zake kuzima kipindi cha matumizi makubwa ya umeme.<br>• Vifaa vya kuzimia moto ni vichache. |

***Chanzo: ZURA, 2025***

***Kiambatisho Namba. 6: Hali ya uingizwaji na matumizi ya Mafuta (Lita) kwa Miezi Tisa (Julai - Machi) 2024/2025***

| MWEZI | | PETROLI | DIZELI | MAFUTA YA TAA | JET A-1 | BUNKER | JUMLA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| JULAI 2024 | Yaliyoingizwa | 8,554,019 | 5,979,496 | 44,479 | 6,137,877 | 0 | **20,715,871** |
| | Matumizi kwa mwezi | 10,035,643 | 6,810,729 | 151,100 | 1,232,000 | 896,100 | **18,229,472** |
| | Wastani wa Matumizi kwa siku | 323,730 | 219,701 | 4,874 | 39,742 | 29,870 | **588,047** |
| AGOSTI 2024 | Yaliyoingizwa | 11,438,076 | 6,258,086 | 0 | 7,400,334 | 0 | **25,096,496** |
| | Matumizi kwa mwezi | 9,825,961 | 6,471,380 | 141,343 | 6,776,000 | 688,863 | **23,214,684** |
| | Wastani wa Matumizi kwa siku | 316,966 | 208,754 | 4,559 | 218,581 | 22,962 | **748,861** |
| SEPTEMBA 2024 | Yaliyoingizwa | 7,548,614 | 5,360,079 | 125,549 | 5,765,239 | 0 | **18,799,481** |
| | Matumizi kwa mwezi | 9,269,358 | 6,075,667 | 95,700 | 4,882,000 | 462,731 | **20,322,725** |
| | Wastani wa Matumzi | 308,979 | 202,522 | 3,190 | 162,733 | 15,424 | **677,424** |
| OKTOBA 2024 | Yaliyoingizwa | 9,910,204 | 7,302,648 | 0 | 1,920,828 | 0 | **19,133,680** |
| | Matumizi kwa mwezi | 10,404,969 | 7,190,913 | 133,800 | 4,305,450 | 0 | **22,035,132** |
| | Wastani wa Matumizi kwa Siku | 359,004 | 227,856 | 6,693 | 152,215 | 19,610 | **765,378** |
| NOVEMBA 2024 | Yaliyoingizwa | 11,057,217 | 7,846,438 | 0 | 6,998,758 | 0 | **25,902,413** |
| | Matumizi kwa mwezi | 9,980,750 | 6,295,422 | 79,316 | 4,622,256 | 444,844 | **21,422,588** |
| | Wastani wa Matumizi kwa Siku | 321,960 | 203,078 | 2,559 | 149,105 | 14,828 | **676,701** |
| DISEMBA | Yaliyoingizwa | 10,515,960 | 6,479,029 | 0 | 3,642,152 | 0 | **20,637,141** |

| MWEZI | | PETROLI | DIZELI | MAFUTA YA TAA | JET A-1 | BUNKER | JUMLA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 2024 | Matumizi kwa mwezi | 10,683,740 | 6,717,807 | 133,690 | 5,727,373 | 501,500 | **23,764,110** |
| | Wastani wa Matumizi kwa Siku | 356,125 | 223,927 | 4,456 | 190,912 | 16,717 | **775,420** |
| **JANUARI 2025** | Yaliyoingizwa | 12,172,602 | 7,616,599 | 0 | 9,004,527 | 0 | **28,793,728** |
| | Matumizi kwa mwezi | 10,717,388 | 7,225,000 | 123,600 | 4,515,000 | 581,950 | **23,162,938** |
| | Wastani wa Matumizi kwa Siku | 357,246 | 240,833 | 4,120 | 150,500 | 19,398 | **772,098** |
| **FEBRUARI 2025** | Yaliyoingizwa | 7,129,216 | 5,538,866 | 184,292 | 3,558,039 | 0 | **16,410,413** |
| | Matumizi kwa mwezi | 9,478,752 | 6,147,034 | 105,100 | 4,480,000 | 409,250 | **20,620,136** |
| | Wastani wa Matumizi kwa Siku | 305,766 | 198,291 | 3,390 | 144,516 | 13,642 | **651,964** |
| **MACHI 2025** | Yaliyoingizwa | 14,561,940 | 9,385,587 | 0 | 3,176,316 | 0 | **27,123,843** |
| | Matumizi kwa mwezi | 10,736,486 | 5,367,755 | 92,000 | 4,389,000 | 419,500 | **21,004,741** |
| | Wastani wa Matumizi kwa Siku | 357,883 | 178,925 | 3,067 | 146,300 | 13,983 | **686,175** |
| **JUMLA YA MAFUTA YALIOINGIZWA** | | **92,887,848** | **61,766,828** | **354,320** | **47,604,070** | **0** | **202,613,066** |
| **JUMLA YA MAFUTA YALIOUZWA** | | **91,133,047** | **58,301,707** | **1,055,649** | **40,929,079** | **4,404,738** | **193,776,526** |

***Chanzo: ZURA, 2025***

**Kiambatisho Namba. 7: Vituo vya mafuta kwa kipindi cha Julai - Machi, 2025**

| | MCHANGANUO WA VITUO | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | WILAYA | GAPCO | UGL | ZPL | PUMA | SERIKALI | BINAFSI | JUMLA |
| UNGUJA | MJINI | 5 | 2 | 2 | | | 3 | **12** |
| | MAGHARIBI "A" | 3 | 3 | 2 | | | 9 | **17** |
| | MAGHARIBI "B" | 1 | 2 | 3 | 1 | | 9 | **16** |
| | KATI | 1 | 3 | 2 | | | 6 | **12** |
| | KUSINI | 0 | 3 | 1 | | | 9 | **13** |
| | KASKAZINI "A" | 2 | 1 | 4 | | | 11 | **18** |
| | KASKAZINI "B" | 1 | 1 | 0 | | | 6 | **8** |
| | JUMLA NDOGO | **13** | **15** | **14** | **1** | **0** | **53** | **96** |
| PEMBA | MICHEWENI | | | | | | 4 | **4** |
| | WETE | | | | | 1 | 4 | **5** |
| | CHAKECHAKE | | | 1 | | 2 | 5 | **8** |
| | MKOANI | | | | | | 4 | **4** |
| | JUMLA NDOGO | | **0** | **1** | **0** | **3** | **17** | **21** |
| JUMLA KUU UNGUJA NA | | **13** | **15** | **15** | **1** | **3** | **70** | **117** |

**Chanzo: ZURA, 2025**

***Kiambatisho Namba. 8: Mwenendo wa bei za Mafuta zilizotangazwa na Mamlaka kwa kipindi cha Julai - Machi, 2025***

| BEI ZILIZOTANGAZWA KWA MIEZI TISA KUANZIA (JULAI HADI MACHI) 2025 | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| MWEZI | TAREHE YAKUTANGAZWA | BEI ILIYOTANGAZWA | | | |
| | | PETROLI | DIZELI | MAFUTA YA NDEGE | MAFUTA YA TAA |
| JULAI | 08.07.2024 | 3,085 | 3,074 | 2,809 | 3,200 |
| AGOSTI | 08.08.2024 | 3,062 | 3,259 | 2,843 | 3,200 |
| SEPTEMBA | 08.09.2024 | 3,164 | 3,247 | 2,837 | 3,200 |
| OKTOBA | 08.10.2024 | 3,008 | 3,111 | 2,827 | 3,200 |
| NOVEMBA | 08.11.2024 | 2,882 | 3,033 | 2,538 | 3,200 |
| DISEMBA | 08.12.2024 | 2,775 | 2,892 | 2,414 | 3,200 |
| JANUARI | 08.01.2025 | 2,775 | 2,892 | 2,414 | 3,200 |
| FEBRUARI | 08.02.2025 | 2,819 | 2,945 | 2,423 | 3,200 |
| MACHI | 08.03.2025 | 2,939 | 3,135 | 2,500 | 3,200 |

***Chanzo: ZURA, 2025***

***Kiambatisho Namba. 9: Gesi iliyoingizwa na kutumika kwa kipindi cha Julai - Machi, 2025***

| MWEZI/KAMPUNI | ORXY GAS TANZANIA LIMITED | | LAKE GAS TANZANIA LIMITED | | TAIFA GAS TANZANIA LIMITED | | ALNABAHAN GAS SUPPLY -O-GAS | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **2024/2025** | **UINGIZAJI** | **MATUMIZI** | **UINGIZAJI** | **MATUMIZI** | **UINGIZAJI** | **MATUMIZI** | **UINGIZAJI** | **MATUMIZ** |
| JULAI | 13,730 | 817,975 | 65,680 | 65,764 | 120,500 | 117,829 | 9,000 | 9,000 |
| AGOSTI | 1,057,222 | 843,364 | 86,780 | 77,139 | 119,590 | 117,829 | 8,000 | 8,000 |
| SEPTEMBA | 850,530 | 843,613 | 86,380 | 74,580 | 118,380 | 120,147 | 8,500 | 8,500 |
| OKTOBA | 1,004,659 | 866,000 | 64,540 | 63,224 | 132,660 | 123,006 | 7,000 | 7,000 |
| NOVEMBA | 1,000,599 | 776,159 | 65,080 | 56,613 | 114,110 | 104,439 | 8,500 | 8,500 |
| DISEMBA | 700,946 | 771,604 | 62,140 | 62,478 | 129,670 | 110,175 | 9,000 | 9,000 |
| JANUARI | 0 | 890,000 | 85,860 | 83,239 | 83,940 | 112,499 | 10,000 | 10,,000 |
| FEBRUARI | 1,037,037 | 798,000 | 66,000 | 64,652 | 125,800 | 100,310 | 10,700 | 10,700 |
| MACHI | 1,154,879 | 895,000 | 64,000 | 71,993 | 100,310 | 150,579 | 12,000 | 12,000 |
| **JUMLA NDOGO** | **6,819,638** | **7,501,715** | **646,940** | **619,682** | **1,044,960** | **1,056,813** | **82,700** | **82,700** |
| | **UINGIZWAJI** | **8,594.238** | | | | | | |
| | **MATUMIZI** | **9,260,910** | | | | | | |

***Chanzo: ZURA, 2025***

***Kiambatisho Namba.10: Tani za Maliasili zilizochukuliwa kwa Kipindi cha Julai – Machi, 2025 Pemba***

| | TANI | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **JINA LA KITUO** | **MCHANGA** | **KIFUSI** | **JIWE** | **KOKOTO** | **TOFALI** | **UDONGO** | **VUMBI** |
| **WILAYA YA CHAKE** | | | | | | | |
| UWANDANI | 0 | 144 | 482 | 0 | 3,641 | 25 | 0 |
| VITONGOJI | 0 | 5475 | 4936 | 5412 | 0 | 32 | 230 |
| FURAHA | 0 | 111 | 103 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| PUJINI | 0 | 2555 | 6043 | 3415 | 0 | 28 | 99 |
| ZIWANI | 4305 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **JUMLA** | **4305** | **8285** | **11564** | **8827** | **3641** | **85** | **329** |
| **WILAYA YA MKOANI** | | | | | | | |
| CHAMBANI | 6263 | 0 | 0 | 0 | 0 | 85 | 0 |
| MUAMBE | 0 | 4415 | 4399 | 2978 | 0 | 72 | 3099 |
| **JUMLA** | **6263** | **4415** | **4399** | **2978** | **0** | **157** | **3099** |
| **WILAYA YA WETE** | | | | | | | |
| KANGAGANI | 0 | 882 | 1657 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **JUMLA** | **0** | **882** | **1657** | **0** | **0** | **0** | **0** |
| **WILAYA YA MICHEWENI** | | | | | | | |
| MICHEWENI | 0 | 5136 | 5971 | 13086 | 3460 | 0 | 2674 |
| CHWAKA TUMBE | 48026 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| WINGWI | 1716 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| SELEMU | 20294 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **JUMLA NDOGO** | **70036** | **5136** | **5971** | **13086** | **3460** | **0** | **2674** |
| **JUMLA KUU** | **80604** | **18718** | **23591** | **24891** | **7101** | **242** | **6102** |

***Kiambatisho Namba. 11: Shughuli zilizotekelezwa kupitia Programu ya Uimarishaji wa Miundombinu ya Maji Zanzibar***

| **Shughuli iliyo pangwa** | **Fedha zilizopangwa kutumika (TZS)** | **Zilizopatikana TZS** | **Utekelezaji Halisi** |
|---|---|---|---|
| Ujenzi wa matangi 11 ya kuhifadhia maji | 14,436,400,000 | 777,226,667 | Malipo yamefanyika kwa ajili ya ununuzi wa Matangi kupitia Kampuni ya "SBS Solution East Africa LTD" iliyopo Kenya. |
| Ununuzi wa Mita na viungio vyake | 1,838,705,340 | 998,988,564 | Malipo ya yamefanyika kwa ajili ya ununuzi wa mita kwa Kampuni ya DANCO na GAMA. |
| Ununuzi wa bomba na vifaa vyake | 5,021,502,316 | 3,220,059,957 | Malipo yamefanyika kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya maji kupitia Kampuni ya YUMUZA na Mashine ya kuungia bomba kupitia Kampuni ya SAPHAIRE. |
| Malipo ya fidia za vipando, mazao na majengo | 1,680,000,000 | 0 | Kazi ya uhakiki wa maeneo yatakayoathirika kwa ajili ya ujenzi wa Miundombinu ya Maji inaendelea. |
| Ujenzi wa Uzio eneo la hifadhi ya maji Bumbwisudi na Vuga mkadini | 1,437,500,000 | 0 | Fedha zinatarajiwa kuhaulishwa kwa ajili ya ununuzi wa bomba za kusafirishia maji. |
| Malipo ya Mfumo wa uangalizi wa miundombinu ya maji | 700,000,000 | 0 | Fedha zinatarajiwa kuhaulishwa kwa ajili ya kazi ya uchimbaji na ufukiaji wa misingi ya bomba. |

| Shughuli iliyo pangwa | Fedha zilizopangwa kutumika (TZS) | Zilizopatikana TZS | Utekelezaji Halisi |
|---|---|---|---|
| Ujenzi wa Vibanda 13 vya kuendeshea Pampu (Unguja 12 kikiwemo kibanda cha Bandamaji, Bandamaji, kwa Hussein Kaani, Kwapweza, Mwera Pongwe, Ubago Nyakurungwi, Makunduchi Mzuri, Kitope Skuli, Dunga Jumba la mawe, Mchangani Mkiwa, Pangeni na (Pemba 1 kibanda cha Jamvini. | 1,698,492,345 | 499,192,376 | Malipo ya fedha kwa ajili ya kazi ya ujenzi wa Vibanda yamekamilika. hatua inayoendelea ni ujenzi wa uzio kupitia Kampuni ya OSAJU. |
| Ununuzi wa Pampu | 1,650,000,000 | 0 | Hatua za kumtafuta mtoa huduma wa ununuzi wa Pampu zinaendelea. |
| **Jumla** | **28,462,600,001** | **5,495,467,564** | **19.3%** |

***Kiambatisho Namba. 12: Shughuli zilizotekelezwa kupitia Mradi wa GiZ Julai-Machi, 2024/2025***

| SN. | Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | % Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Kusimamia na kuandaa utekelezaji wa Sera na Miongozo inayohusiana na sekta ya maji safi na usafi wa mazingira; | Asilimia ya Sera na miongozo iliyoandaliwa | 100 | 10 | 15 | • Mradi unaendelea na hatua za kumuajiri Mshaurielekezi kwa ajili ya kazi kuandaa mikakati ya utekelezaji wa Sera, Miongozo na Mikakati inayohusiana na sekta ya maji safi na usafi wa mazingira.<br>• Kuendelea na zoezi la ukusanyaji wa taarifa kwa wadau kuhusiana na uwekaji wa bei za maji safi na usafi wa mazingira (Water and Sanitation Tarrif).<br>• Mradi unaendelea na hatua ya ununuzi wa mkandarassi kwa ajili ya kazi za uwekaji wa pampu za solar katika visima.<br>• Utayarishaji wa mkakati wa mafunzo kwa watendaji wa ZAWA/RANDWATER kwa Taasisi ya Global Water Center |

| SN. | Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | % Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | na Oikos .<br>Utayarishaji wa mkakati wa masharikiano ya kuijengea uwezo baina ya ZAWA/RANDWATER na Taasisi za Maji kutoka Ujerumani za Gelsenwasser and OOWV. |
| 2. | Kuanzisha mifumo ya ukusanyaji, uchambuzi na ufuatiliaji wa taarifa zinazohusiana na rasilimali maji iliyopo chini ya ardhi. | Asilimia ya mifumo iliyoanzishwa | 100 | 10 | 10 | Mradi unaendelea na hatua za kumuajiri Mshaurielekezi kwa ajili ya kazi kuandaa mikakati ya utekelezaji wa Sera, Miongozo na Mikakati inayohusiana na sekta ya maji safi na usafi wa mazingira. |
| 3. | Kufanya Upembuzi Yakinifu kuweza kuvuna maji ya mvua kama chanzo mbadala cha maji; | Asilimia ya Upembuzi Yakinifu iliyofanyika | 100 | 10 | 15 | • Mradi unaendelea na hatua za kumuajiri Mshaurielekezi kwa ajili ya kazi kuandaa mikakati ya utekelezaji wa Sera, Miongozo na Mikakati inayohusiana na sekta ya maji safi na usafi wa mazingira.<br>• Kuendelea na zoezi la ukusanyaji wa taarifa kwa Kamisheni ya Utalii na Jumuiya ya Wawekezaji wa Mahoteli (ZATI) |

| SN. | Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | % Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | kuhusiana na uvunaji maji ya mvua kama chanzo mbadala cha maji, matumizi bora ya maji sambamba na kuwajengea uwezo wadau. |
| 4. | Kuratibu ujumuishaji wa masuala ya kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi na jinsia katika usimamizi wa rasilimali maji; | Asilimia ya uratibu iliyofikiwa | 100 | 10 | 10 | Mradi unaendelea na hatua za kumuajiri Mshaurielekezi kwa ajili ya kazi kuandaa mikakati jumuishi wa masuala ya kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi na jinsia katika usimamizi wa rasilimali maji. |
| 5. | Kuandaa mipaka katika maeneo ya vyanzo na vianzio vya maji. | Asilimia ya mipaka iliyoandaliwa | 100 | 10 | 10 | Mradi unaendelea na hatua za kumuajiri Mshaurielekezi kwa ajili ya kazi kuandaa na kuyatambua maeneo ya vyanzo vya maji (Catchement areas). |

**Kiambatisho Namba. 13: Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026**

| | KAZI ZA KAWAIDA | | | KAZI ZA MAENDELEO | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **PROGRAMU KUU/PROGRAMU NDOGO** | **MSHAHARA** | **RUZUKU YA MSHAHARA** | **UENDESHAJI WA OFISI (OC)** | **MAKISIO YA SMZ** | **MHISANI** | **RUZUKU** | **MAPEMDEKEZO YA 2025/2026** |
| **USIMAMIZI WA HUDUMA ZA MAJI** | **307,435,000** | **10,110,400,000** | **543,010,000** | **25,034,560,000** | **53,599,745,000** | **75,923,484,000** | **165,518,634,000** |
| Usimamizi na Uratibu wa Huduma za Maji | 307,435,000 | 10,110,400,000 | 543,010,000 | 25,034,560,000 | 53,599,745,000 | 75,923,484,000 | **165,518,634,000** |
| **USIMAMIZI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MADINI** | **889,116,000** | **-** | **316,783,000** | **40,355,685,000** | **10,443,290,000** | **-** | **52,004,874,000** |
| Usimamizi na Uimarishaji wa Huduma za Nishati | 889,116,000 | - | 272,582,000 | 40,355,685,000 | 10,443,290,000 | - | **51,960,673,000** |
| Usimamizi na Uimarishaji wa Huduma za Madini | - | - | 44,201,000 | - | - | - | **44,201,000** |
| **UENDESHAJI NA URATIBU WA MIPANGO YA WMNM** | **1,724,049,000** | **-** | **1,578,207,000** | **-** | **-** | **-** | **3,302,256,000** |
| Utawala na Uendeshaji wa WMNM | 792,434,000 | - | 568,231,000 | - | - | - | **1,360,665,000** |
| Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za | 156,207,000 | - | 603,655,000 | - | - | - | **759,862,000** |

| KAZI ZA KAWAIDA | | | | KAZI ZA MAENDELEO | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **PROGRAMU KUU/PROGRAMU NDOGO** | **MSHAHARA** | **RUZUKU YA MSHAHARA** | **UENDESHAJI WA OFISI (OC)** | **MAKISIO YA SMZ** | **MHISANI** | **RUZUKU** | **MAPEMDEKEZO YA 2025/2026** |
| WMNM | | | | | | | |
| Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za WMNM - PEMBA | 775,408,000 | - | 406,321,000 | - | - | - | **1,181,729,000** |
| **JUMLA KUU** | **2,920,600,000** | **10,110,400,000** | **2,438,000,000** | **65,390,245,000** | **64,043,035,000** | **75,923,484,000** | **220,825,764,000** |

Zanzibar Government Printing Press Agency